

YEHOVA-YIRE

 Hebu na tuendeleo kusimama kwa muda kidogo tu, tunapokutana na Mungu katika maombi. Ni wangapi walio na haja, leo? Je, waweza kuacha tu ijulikane kwa mkono ulioinuliwa? Hebu tumwamini sasa, tunapoomba.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa yale macho yetu yameona, na masikio yetu yamesikia, ufunuo wa Yesu Kristo kwa watu Wake, na kuwa na majaliwa ya kuishi katika siku hii ambayo wazee wetu wote, na manabii, mitume, na watu mashuhuri katika miaka iliyopita wametamani kuiona siku hii. Laiti wangeweza tu kujitokeza jukwaani, hao manabii wa kale, na kuona jambo lile lile waliloona katika miaka hiyo sasa likitendeka, kungekuwa na ibada za kiinjalisti jinsi gani! Labda, wamefungiwa gerezeni, wanawaita “wendawazimu.” Tunaishi katika siku ya kuona haya yote waliyoyaona kwa imani.

³ Mungu, jalia tuchukue hii nafasi wakati imewasilishwa kwetu. Wao wanatutegemea sisi, waliacha Neno lao, Neno la Mungu waliloonyeshwa, wanatutegemea sisi kulitekeleza. Yesu alikuja kulithibitisha, na kumtuma Roho Mtakatifu kuendeleza hizi kazi na kutupa nguvu za kufanyia kazi, mpaka mambo haya yote yatimizwe, na ndipo Kanisa kuu lililokombolewa la Mungu aliye hai linyakuliwe kumlaki.

⁴ Kuna wengine hapa leo, Baba, ambao hawana tumaini hili la baraka, tulivu nafsini mwao, jalia hii iwe ndiyo siku ambayo watalipokea. Huenda kukawa na wale hapa ambao wamechoka njiani, hebu wajue, Bwana, ya kwamba kamwe hatuji kwenye mandari, bali kwenye uwanja wa vita, kupigania kila inchi ya njia, wape ujasiri, watie nguvu.

⁵ Wapo wengine hapa ambao wamejeruhiwa, Bwana, adui amewarushia mishale ya maradhi mwilini mwao, na mateso. Kuna mashujaa waliolala hapa kwenye uwanja wa vita, ambao wangukuwa wameamka na kwenda kama wangeweza, lakini wao ni, lazima wapelekwe kwenye nyumba ya wageni ambamo Mwangelizi atashughulika. Baba, jalia gari la Mungu la kuchukulia wagonjwa liwapeleke kwenye imani halisi, ya kweli alasiri ya leo, tujalie, Bwana, tunaomba ya kwamba wataponywa.

⁶ Kulikuwa na wengine walioinua mikono yao, Bwana, ambao sijui shida zao zilikuwa nini, ama shauku yao ni nini, chochote kile, ninawaombea, Baba, ya kwamba utawajalia haja yao. Jipatie utukufu kutokana na hii ibada tunapojiwasilisha wenyewe na, Injili yetu uliyotuachia kukuhubiria Wewe kwa kazi zaidi katika thibitisho. Katika Jina la Yesu. Amina.

⁷ Mwaweza kuketi. Kwa kweli ninasema kwamba ninasikitika ya kwamba hii ndiyo ibada ya kumalizia uamsho huu mdogo, ama ninii tu, hatujawa na wakati wa uamsho, maskini kusanyiko letu. Lakini nimekuja kwa mwaliko wa kundi hili zuri la watu, wahudumu wa mjini, na kila mahali, kwa sababu nilijisikia kuongozwa kuja. Kuna mahali panapongojea, sisemi hili ili tu kulisema, ninalisema kwa sababu ni kweli, kuna mahali panapongojea ambapo pana makumi elfu ya watu pamoja, kote ng'ambo. Mamia ya mahali huko ng'ambo, miji mikubwa Marekani, kote. Lakini kwa kawaida mimi huanika vitu hivyo, mialiko, na kuiombea, haijalishi ni wapi, popote Bwana anaposema niende, ninaenda.

⁸ Hapa tu wakati fulani uliopita, nilisoma mwaliko, mimi na mke wangu tulikuwa tukipata mialiko, nyumbani, mtu mmoja akasema, "Ndugu Branham, kama utakuja, tutakuhakikishia pesa *kadhaa wa kadhaa*," mwajua, "na *kadhaa* iwapo utakuja tu."

⁹ Barua iliyofuata ilisema, "Ndugu Branham, sina kitu ninachoweza kukuahidi, si hata mahali pa kulaza kichwa chako." Kasema, "Mimi ni mtu aliyeoa, nina binti saba, na watano kati yao ni watu wazima, sote tuko hapa katika nyumba ndogo, yenye vyumba vitatu." Kasema, "Ninahubiri chini ya misonobari miwili." Kasema, "Mungu anajua ninakuhitaji." Mnajua nilikoenda? Huko chini, hiyo ni kweli. Na huko, kutoka kwenye mkutano huo, wakajenga ma—maskani *kubwa*, naye mtu huyo, nijuavyo mimi, angali ni mchungaji wake. Na hiyo ilikuwa huko chini Arkansas. Mnaona, daima ni bora zaidi kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu.

¹⁰ Kamwe sijwahi kuhubiria ku—kusanyiko zuri kuliko lile nimekuwa nalo siku hizi tano usiku, siku tano hapa. Ninawathamini ninyi nyote, mmekuwa waaminifu sana. Ninathamini kundi hili zuri la wahudumu hapa nyuma. Nina furaha sana ya kwamba—ya kwamba kundi hili la watu lina wachungaji wa kuwalinda, namna hii.

¹¹ Kweli, *mchungaji* linatokana na neno, *mlishaji*, "mlishaji wa kundi." Nao ni wachungaji, walishaji. Nayo Injili hii ninayohubiri, wanaiamini, hiyo ndiyo sababu wanaidhamini. Hiyo ndiyo sababu wameketi hapa juu jukwaani kusema ya kwamba "Tunauwakilisha mkutano huu."

¹² Nami, waongofu, watu ambao wametoa maisha yao kwa Kristo, na huduma yao ya baadaye, ninatumaini ya kwamba kwa vyovyote vile mtawaona baadhi ya hawa wahudumu, na kuwaacha wawabatize katika imani ya Kikristo. Na—naye Mungu awape Roho Mtakatifu, nawe uwe mfuasi wa kanisa lao.

Sasa, hatuwakilishi shirika lolote, ama ninii fulani... Tunaninii tu, Yesu Kristo, sisi sote.

¹³ Ninataka kuwashukuru kwa kunialika, kwa kusimama pamoja nami na kunisaidia. Ndugu, hakika ninawathamini. Nami naomba ya kwamba siku moja, kama ni mapenzi ya Mungu, ninaweza kurudi kwa ajili ya mkutano mrefu zaidi ambapo tunaweza kuingia mahali fulani, na kuwa na muda zaidi.

¹⁴ Na kwa maafisa, wadhamini wa jengo hili ambao wameturuhusu kuchukua jengo hili, tunathamini hilo, kwa heshima ya waangalizi, na kadhalika, na yote waliyofanya. Mmoja wa hao wavulana alikuwa amesimama huko nje sasa hivi, akatuwekea mahali pa kuegeshea magari, mzuri sana, mwungwana wa aina nzuri anayesimama pale, mvulana mweusi, ninamtakia baraka za Mungu zilizo bora sana. Na yote, ninayathamini.

¹⁵ Na kwa ajili ya kusanyiko, jinsi mlivyoitikia na kuliadini Neno ambalo limehubiriwa!

¹⁶ Nao wananiambia ya kwamba madeni yote yalilipwa, na kwamba walichukua sadaka ya upendo. Mimi, haikunibidi kufanya hivyo, ninathamini hilo, hata hivyo. Nami nitawahakikishia ya kwamba hakutakuwa na yoyote ya hizo itakayotumika kwa wiski, sigara; zitaingia moja kwa moja katika Ufalme wa Mungu. Ninachofanya nazo, zinaenda moja kwa moja kwenye. . . Mnajua kinachozipata? Zinaenda kwenye misheni za kigeni, sichukui hata peni yake, zinaenda kusaidea misheni ambako ninaenda ng'ambo. Ninapoweka akiba ya kutosha, basi ninaenda ng'ambo na kuwahubiria watu ambao hata hawajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, hawajui mlo mzuri ni nini, hata hawavai nguo.

¹⁷ Kwa hiyo sina budi kuwajibika kwa ajili ya pesa hizo, na ndipo ninajua, mimi ni msimamizi mzuri, nitazitumia katika Ufalme wa Mungu. Kanisa langu hunipa m—mshahara wa dola mia moja kwa juma, hizo ndizo ninazotumia pamoja na watoto wangu.

¹⁸ Jambo lingine, mtu fulani alinitumia dola mbili, ninathamini hilo, kwa mwanangu, na kulikuwa na hundi mbili za dola tano zilizoingia juma hili. Na ninii. . . Mtu mmoja muda mfupi uliopita alitutumia kifurushi cha maforosadi meusi yaliyotiwa koponi, mke wangu bado hajui hilo. Mpenzi, popote ulipo, tunaelekea kwenye yubile ya ulaji bora sasa. Na—napenda sana maforosadi meusi.

¹⁹ Baadhi yenu, labda, mliniandikia barua, nilijibu vizuri nilivyoweza. Sasa, kwa maswali mnayoniuliza katika Mafundisho, niliwarudisha tu kwa mchungaji wenu, mnaona, kwa sababu si—sifanyi hivyo, mnaona. Ni vizuri, ninawathamini kwa kuweka imani kama hiyo, lakini mnaona, sisi sote tusingekubaliana, tu, juu ya mambo ya msingi sisi sote, tunakubaliana mambo yale yale, lakini kila mtu, labda wawili

au watatu wanaoketi *hapo* wasingeweza. Hiyo ndiyo sababu nilisema, “Mwulizeni mchungaji wenu,” mnaona, kwa sababu wakati mwingine husababisha mzozo kidogo kanisani, nasi hatutaki hilo, tu—tunataka mwe na upatanifu na moyo mmoja. Ninamwazia mchungaji wenu kama ule wimbo, *Neema ya Ajabu*:

Neema ndiyo iliyonileta salama umbali huu,
Neema itanipeleka mbele.

²⁰ Kama mchungaji amehubiri Injili, nanyi mmeongoka na kujazwa na Roho Mtakatifu, endeleeni kumwamini Yeye, atayashughulikia yaliyosalia, aendelee tu mbele moja kwa moja.

²¹ Kwa hiyo, mimi sijibu maswali ya Mafundisho. Ninaamini tu katika lile Fundisho kuu la kimsingi, la kiinjalisti la Biblia. Na yale ninayosema hapa, hata kama mchungaji wenu hakubaliani nayo, tutajua tu jambo moja, kwamba kimsingi, sote wawili tunaamini jambo lile lile.

²² Mwajua, hata mimi na mke wangu hatukubaliani juu ya kila kitu. Hiyo ni kweli. Yeye, anapokula sambusa, anapenda sambusa ya forosadi, nami napenda sambusa ya cheri. Ninapenda kunywa cheri, na ninapenda sambusa ya forosadi pia, naelewa, lakini hula sambusa ya cheri, ninaimwagilia maji hayo ya matunda juu yake, kisha ninamwagilia siagi juu yake, kisha sukari ya rojorojo juu ya hiyo, iko tu tayari kuliwa basi, hiyo ni kweli, ni nzuri *kweli*.

²³ Sasa, nawaambia, yeye anapenda kitu kile kile, bali anaogopa kalori, nadhani hiyo ndiyo. Lakini nakwambia, Mpenzi, popote ulipo humu ndani, tutakapopika pai hii ya forosadi, nitakutolea kalori zote humo, u—utakuwa tu na wakati mzuri.

²⁴ Mungu awabariki, asanteni sana, kila kitu ambacho mmefanya, mliunga mkono mikutano na hilo tu ndilo lililohitajika. Nitawaomba fadhili moja zaidi, mkiweza. Labda msimu huu wa kiangazi, na kwenye... Natumaini kuwaona tena ng'ambo hii ya Yordani, nisipowaona, nitakutana nanyi Ng'ambo ya pili, na Injili ii hii ambayo nimekuwa nikihubiri, nitasimama nihukumiwe kwayo huko Ng'ambo.

²⁵ Sasa, ningetaka kusema jambo hili, ya kwamba kama kuna wakati wovote ninaoweza kuwafadhili, ningefurahia kufanya hivyo. Nilizoea kusema, “Ningeninii, usiku kamwe huingii giza sana, mvua kamwe hainyeshi sana, hata nisiweze kutambaa niwafikie.” Sasa, pamoja na huduma ya ulimwenguni kote, mawasiliano ya kibinafsi ya watu wapatao milioni kumi, nisingeweza kufanya hivyo. Maana tulikuwa na simu moja, wakati mmoja tulihasabu simu zilizoingia kwenye simu hii moja, nazo kwa wastani zilikuwa, naamini zilikuwa, yapata simu ishirini ama thelathini za mbali kwa saa. Mnaona? Kwa hiyo mnaona, usingeninii tu, usingeweza kuzijibu zote, na kuzifikia.

²⁶ Lakini ninasema jambo moja, ninafanya kila niwezalo. Wanaandika haja hizo, nikiweza, wengi niwezao kuwapigia, nawapigia, na kumwombea kila mmoja wao, na kila kitu niwezacho kufanya. Nasi tunaombea vitambaa vidogo na kuvituma, ukitaka kimoja, kila kitu tulicho nacho ni bure, kwa hiyo agizia tu na kukichukua.

²⁷ Sasa, hatutaki anwani yako, kama nilivyosema, nina wakati mgumu kupata usaidizi hata wa kujibu barua. Sasa, utapata ki—kipande kilichotengenezwa, kipande kilichorudufiwa, kuhusu jambo la kufanya, jinsi ya kumwendea mchungaji wako, unapopata kitambaa hiki kidogo. Ni wangapi wanaoamini hilo, leso na nguo, Matendo 19? Na hiyo—hiyo ni, sehemu iliyo kuu sana ya huduma yangu ni hiyo.

²⁸ Nami sikuzote nilirejea hili, linaonekana la ajabu sana. Kulikuwa na maskini mwanamke mmoja huko Ujerumani aliyechukua kimoja hapa, yapata mwaka mmoja ama miwili iliyopita. Loo, alikuwa ametafsiri upande wa nyuma, mfasiri alifasiri, katika Kiingereza, kwa hiyo ningeweza kuisoma. Alikuwa amelemaa kwenye kiti cha magurudumu kwa yapata miaka kumi na mitano. Naye akapata hiki, naye akasoma jinsi ambavyo hana budi kumwita mchungaji, na iwapo mchungaji hakuwapo, awaite Wakristo kadhaa, kisha akiri kila kosa alilowahi kufanya halafu ajiweke sawa na Mungu, kisha akiweke juu ya moyo wake, akifunge kwenye vazi lake la ndani, na kuamini.

²⁹ Kwa hiyo alipofanya haya yote, mchungaji wake alikuwa pale, naye akakiweka moyoni mwake, akasema, “Sasa, ewe mzee ibilisi, umenisumbua muda mrefu vya kutosha, ondoka!” Huyo akasimama, akaenda zake akitembea. Kweli. Hivyo ndivyo—ndivyo tu ilivyokuwa rahisi, ameponywa kikamilifu, mzima.

³⁰ Ni imani yako rahisi tu katika kuamini. Watu hujaribu kuifanya imani kuwa ni ngumu sana, si ngumu, ni imani rahisi tu, ya kitoto.

³¹ Mnajua, damu katika Agano la Kale ilipakwa kwa hisopo, mmesikia hilo mara nyingi. Mnajua hisopo ni nini? Magugu tu ya kawaida, unayapata popote. Huko chini Misri, na kadhalika, inakua kwenye matofali ya udongo, nyufa katika jengo, ambapo u—upepo umeipeperushia mbegu. Wanachuna hilo, maskini jani dogo lenye umbo la almasi, lina ua juu yake, hisopo tu, ya kawaida. Inamaanisha nini? Haikubidi kuwa na imani yoyote kuu kupaka Damu ya Yesu Kristo, imani ya kawaida tu, liamini. Hivyo tu.

³² Basi kumbukeni, Neno la Mungu litamshinda Shetani mahali popote, wakati wowote, kwenye msingi wowote. Hiyo ni kweli. Neno la Mungu litamshinda Shetani.

³³ Sasa, swali, jambo nililotaka kuwaulizeni: Ninakabiliwa na magumu mengi sana, nchi za kigeni, nikikabiliwa na—na

kila namna ya fundisho la ibilisi ambalo lingeweza kuwaziwa. Wakati pepo zinapovuma kwa nguvu sana na joto, wamishenari wamesimama, wakitaka kuona ni kitu gani kinachokaribia kutukia, wao, wachawi wote wakinizunguka, hivi naweza kukumbuka huko Richmond, Virginia, mnaniombea? Je, naweza kukumbuka hilo? Hilo ndilo ninalotegemea. Mungu awabariki. Nitakuwa nikitegemea hilo, daima nitaikumbuka Richmond, kundi hili dogo, zuri.

³⁴ Sasa, juma lijalo tuko hapa Middletown, Ohio. Halafu basi kwa mialiko yenu yote, ndugu huyu, baadhi, mmoja wa hao ndugu alikuwa hapa mahali fulani, ndiyo kwanza niichukue, niliiona muda mfupi uliopita wakati katibu wangu wa hudumani aliponipa nikirudi, hapa juu, kwenye hii Washington, DC, tena. Sasa, huenda tukaweza kulishika hilo hivi karibuni sana, nilijisikia nigusie hilo kidogo, huko Washington, DC labda, kabla ya kwenda ng'ambo, kwa hiyo huenda tukaweza kuuchukua huo.

³⁵ Na kwa huyo ndugu, sidhani yuko hapa, alikuwa mkutanoni jana, kuhusu huko chini Carolina, sina budi kwenda Florida, mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo, ninapaswa kuhutubia huo Julai, naamini, mosi, tarehe mbili, tatu, na nne, huko Miami, na halafu, labda, nikishuka kwenda, huenda nikaweza kuchukua huo, mmojawapo huko Carolina, tukishuka, maana wanapitia Barabara Kuu ya 1 wapate kushuka.

³⁶ Bwana awabariki. Ningeweza tu kuzungumza nanyi alasiri nzima, lakini hamna budi kwenda kanisani usiku wa leo, nami natumaini mtaenda, na mtakuwa na mkutano mkubwa sana, sana.

Sasa, hebu, mara nyingine tena, tumwinamishie Mungu vichwa vyetu.

³⁷ Baba, tunajiandaa kufungua kurasa za Kitabu hiki. Nasi tunasoma katika Biblia ambapo tuliona Kitabu hiki kwenye mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi, wala hapakuwapo na mtu aliyeweza kukitwaa hicho Kitabu, wala kuifungua Mihuri, wala hata kukiangalia. Lakini alikuja Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Naye akakitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi, naye akakifungua kile Kitabu na ile Mihuri.

³⁸ Tungeomba leo hii, Baba, tunajua mtu yeyote ambaye kimwili anaweza kuinua mkono wake angeweza kufungua kurasa za Kitabu hiki, bali hakuna mtu anayeweza kukifungua, ila Mwana-Kondoo yuyo huyo, tunaomba ya kwamba atatujalia alasiri ya leo, kwamba atakuja na kutufungulia Injili hii. Na tutakapoondoka alasiri ya leo, na ibada zimefungwa, na tuseme, kama wale waliokuwa wakitoka Emau siku ile, "Je, mioyo yetu

haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁹ Bwana awabariki.

⁴⁰ Na sasa, ninyi mnaoweka kumbukumbu za Maandiko ya mahali tunapozungumzia, kama mngefungua mlango wa 22 wa Mwanzo na kifungu cha 14:

Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire: kama watu wasemavyo hadi leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana.

⁴¹ *Yehova-Yire.* Mungu ana Majina saba ambatani, ya ukombozi, nalo *Yehova-yire* ndilo Lake la kwanza, "Bwana atatoa dhabihu," *Yehova-rafa*, "Bwana akuponyaye magonjwa yako yote," na *Yehova*... "bendera yako na ngao yako," na kadhalika. Yeye ana Majina saba ambatani, ya ukombozi, na Majina hayo hayatenganiki.

⁴² Usiku ule, wakati picha ile ilipopigwa, mnayo hapa sasa, ambayo imesifika ulimwenguni kote, ya ile Nguzo ya Moto iliyokuwa imesimama mahali nilipokuwa, na ninii... Wameipiga mara nyingi, nyingi, lakini tusingeiacha itangazwe mpaka ilipohakikishwa; kama vile ushuhuda wa baadhi ya uponyaji.

⁴³ Hivi mliona katika Wafanyabiashara Wakristo, kile kitabu kidogo mlichosambaziwa hapa, *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo, kuhusu kufufuliwa kwa wafu? Hatuwezi kusema hivyo isipokuwa kiwepo cheti kilichoidhinishwa na daktari. Mnaona? Na hicho hakina budi kuthibitishwa kabla hujakichapisha, kitu chochote kama hicho, kwa sababu ni haramu kufanya hivyo. Kwa hiyo, vema mambo haya ni ya kweli.

⁴⁴ Na sasa, hiyo Nguzo ya Moto iliyo kwenye hiyo picha, usiku ule ilipopigwa ilikuwa ni huko—huko Houston, kwenye Ukumbi wa Michezo wa Sam Houston. Tulikuwa na yapata watu elfu nane kwenye Ukumbi wa Muziki, nasi tukaenda kule usiku huo tukiwa na yapata elfu thelathini na mbili. Lakini walikuwa wameniomba, kama mhudumu wa Kibaptisti, kufanya mdahalo pamoja naye juu ya uponyaji wa Kiungu. Sifanyi mdahalo na watu, siamini katika kuzozana na watu, Injili haikufanywa iwe ya kuzozaniwa.

⁴⁵ Loo, nilipowekwa wakfu kwa mara ya kwanza katika kanisa la Kibaptisti, nilifikiri nilikuwa mtetezi wa imani. Kwa hiyo nikaona, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja." Kwa hiyo, mnaona, mbona, u—u—ubishane na watu, wao—wao wameng'ang'ania njia zao, la sivyo wasingekuwa wakibishana, kwa hiyo basi, hu—huwafanyi kuwa bora zaidi.

⁴⁶ Kwa hiyo alitaka nichukue usiku mmoja kufanya mdahalo. Ndio li—lile *Houston Chronicle*, ama, ninaamini hilo lilikuwa

ndilo jina la hilo gazeti, waliliandika, naye akaweka tangazo la kulipwa mle ndani, na kusema tulichofanyiziwa, tuliogopa kuikabili Injili kwa Neno la Mungu.

⁴⁷ Kwa hiyo Dk. F. F. Bosworth, wakati huo alikuwa na umri wa kama miaka themanini, akapanda juu pale. Nao waandishi wa habari walikuwa wakingojea, wakasema kile nilichokuwa ninaenda kusema juu yake, nami nikasema, “Mimi sibishani. Mimi . . . Hiyo . . . Nina usiku *kadha* tu wa kuwa hapa, nami nina siku mbili zaidi usiku uliosalia, na kuna makumi ya maelfu ya watu hapa wa kuombewa, kwa nini nipoteze usiku mmoja kwa mkosoaji mmoja? Mwacheni aendeleo, Yesu alisema, ‘Waachen. Kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, hivi hawataanguka shimoni?’” Nikasema, “Hawa hapa maelfu wanaoamini, kwa nini kujipumbaza na mmoja asiyeamini,” mnaona, “na kupoteza muda huo wote?”

⁴⁸ Ndugu Bosworth, kamwe sitasahau ninii . . . Yuko utukufuni leo, umri wa miaka themanini. Naye Dk. Best wa maskani ya Kibaptisti alikuwa ndio kwanza atoke shuleni, na yapata umri wa miaka thelathini, pamoja na digrii zake zote, na kadhalika. Ndipo Ndugu Bosworth akasema, “Vema, Ndugu Branham, kama hutaki kuufanya, hebu niufanye.” Nikawaza juu ya maskini Kalebu, “Hebu niuchukue mlima huu.”

Nikasema, “Ukiahidi hutabishana.”

Akasema, “Ninaahidi.” Naye huyo akaenda.

⁴⁹ Na hapa, kesho yake, bila shaka mnajua jinsi magazeti yanavyoweza kuutania, “Unyoya wa kikanisa utarushwa.” Kwa hiyo basi hilo lililivutia kundi kubwa.

⁵⁰ Basi huo ni wakati mmoja, ndugu, ambapo niliona ya kwamba Wapentekoste wote watakuwa na nia moja, siku moja. Sijali walikuwa wamepanda ngamia wangapi wenye manundu, moja, mbili, tatu, nne, wote walikuwa pale, kwa sababu kitu kimoja shirika, Uponyaji wa Kiungu ulikuwa hatarini, nao wote wanauamini huo. Naam, bwana. Nao hawa hapa wote.

⁵¹ Basi usiku huo wakati Dk. Best aliposimama, alitaka Ndugu Bosworth atangulie. Basi Ndugu Bosworth akasema, “Nina maswali mia sita yaliyoandikwa hapa kwenye karatasi. Daktari Best, maswali haya yanathibitisha ya kwamba msimamo wa Kristo, leo, kwa wagonjwa, ni kama tu ulivyokuwa wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Kama unaweza kuchukua moja ya maswali haya na kuyakanusha kwa Biblia, basi nitaenda pale na kuketi chini, na—na tutasema umeshinda huu mdahalo.” Hilo ni tamshi pana sana, lakini yeye, mvulana huyo alijua kutojipumbaza na jamaa huyo.

Lo, akasema—akasema, “Nitalishughulikia hilo nitakapofika hapo juu, nitalishughulikia hilo nitakapofika hapo.”

⁵² Akasema, “Basi, Bw. Best,” akauliza msimamizi, kasema, “Nitakuuliza swali moja, ujibu, *ndiyo*, au, *la*, nami nitaketi chini, endapo tu utasema, *ndiyo*, au *la*.”

Na, msimamizi, akasema atafanya hivyo.

⁵³ Akasema, “Je, yale Majina saba ambatani ya Yehova ya ukombozi yalitumika kwa Yesu, *ndiyo*, au *la*?” Loo, jamani!

⁵⁴ Sasa, sikupaswa kuwa pale, bali nilikuwa nimeketi kwenye roshani ya kumi huko juu, mahali fulani, nimevaa koti langu, polisi wawili wamesimama juu yangu namna *hiyo*, na ndugu yangu, na mke, na binti yangu mdogo, wameketi pale. Nawaambia, nilihisi mitetemeko ikipita! Sikuwa nimewahi kuwazia hilo hapo kabla maishani mwangu. Asingeweza kulijibu hilo. Mnaona?

⁵⁵ Kama ambatani, Majina ambatani ya Yehova ya ukombozi, hayakutumika kwa Yesu, Yeye hakuwa Yehova-Yire, “Dhabihu iliyotolewa na Bwana,” Yeye hakuwa Mwokozi. La, bwana. Na kama lilitumika Kwake, basi Yeye ni Yehova-Rafa kadiri tu Yeye alivyo Yehova-Yire, kwa sababu hayo Majina hayatenganiki. Yehova, Mponyaji, kadiri Yeye alivyo Mwokozi, hilo lilitosha. Loo!

Ndipo akasimama, akasema, “Nitalishughulikia...” Asingemjibu *ndiyo*, ama *la*, kwa hiyo asingeweza kumjibu.

⁵⁶ Kwa hiyo nikawazia, “Yule shujaa, yule mzee aliyesimama pale!” Kwa hiyo basi akapanda kule, ndipo akahubiri mahubiri mazuri sana ya Kikampbeli. Nilipembeza katika kitanda kidogo cha Kibaptisti, ninajua wanachoamini. Kwa hiyo kamwe hakuhubiri fundisho la Kibaptisti, alihubiri uponyaji wa Kiungu katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Ungehitajiye uponyaji wa Kiungu katika ule Utawala wa Miaka Elfu wakati wana mwili uliotukuzwa? Loo, kile yeye—kile anaenda... Jinsi watu watakavyojaribu kuyavuruga Maandiko kwa sababu tu hawayajui, ama, hawatamruhusu Roho Mtakatifu awaongoze kwake! Hiyo ni kweli.

⁵⁷ Kwa hiyo basi, alipomaliza, aliwaambia, alikuwa na baadhi ya wapiga picha wa Studio za Douglas, akasema, “Nataka mnipige picha sita.” Akasema—akasema, “Nitamchuna ngozi mzee huyo, Bosworth, na kuanika ngozi yake kwenye mlango wangu wa kusomea, kama kumbukumbu ya uponyaji wa Kiungu.” Msimamo huo ulionyesha ya kwamba kulikuwa na kasoro *hapa* chini kwa ndugu Mkristo. Lakini Bwana ndiye Ulinzi wetu.

Ndipo akakunja ngumi yake namna *hii*, akasema, “Sasa, ipigeni *hivi*.” Ndipo wakaipiga. Wakapiga picha sita.

⁵⁸ Sasa, nilipokuja jukwaani, kama mkiangalia, kama kamwe wakianza kupiga, hawatawaruhusu wapige picha kwa kuwa, ile—ile Nuru ninayoangalia ni nuru, ni nuru, pia.

⁵⁹ Kwa hiyo, na kwa hiyo—kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, akasema, Bw. Best, walikuwa na kidimbwi wakati huo, kwa hiyo basi akasema, “Hakuna mtu anayeamini katika uponyaji wa Kiungu, ila kundi la watakatifu wanaojibingirisha.” Kisha kasema, “Hakuna mtu angeamini upuuzi kama huo.”

Bw. Bosworth akasema, “Bw. Best, sa—samahani, makanisa yote yanaamini katika uponyaji wa Kiungu iwapo yanaamini Biblia.”

Akasema, “Vema,” akasema, “Mbaptisti m—mzuri asingeamini upuuzi kama huo.”

Akasema, “Hebu kidogo, Bw. Best.”

Akamwambia msimamizi, “Hivi naweza kuchukua maikrofoni kwa dakika moja?” Akasema angeweza.

⁶⁰ Kasema, “Watu wote katika jumba hili la mikutano,” yapata watu ishirini na mbili elfu, akasema, “ninyi watu wote humu ndani ambao ni wafuasi wa makanisa haya ya Baptisti, pamoja na hawa wahudumu wa Baptisti walioketi hapa, ambao ni wafuasi wa makanisa haya ya Baptisti wanaoweza kuonyesha kwa cheti kwamba mumeponywa kwa uponyaji wa Kiungu tangu Ndugu Branham amekuwa hapa, simameni kwa miguu yenu.” Ndipo watu mia tatu na kitu wakasimama.

Kasema, “Vipi kuhusu hilo?”

⁶¹ Akaketi pale, kisha akasema, “Mleteni mponyaji huyo, hebu nimwone akifanya. Hebu... Leteni mbe-... Hebu nimwone, hawezi kunipumbaza akili,” namna hiyo. Ndipo akaanza kuondoka jukwaani, kasema, “Hebu nimwone akifanya.”

Kasema, “Jionee aibu, Bw. Best! Hupaswi kusema hivyo.”

Kwa hiyo, akaanza kuondoka jukwaani.

⁶² Ndipo akasema, “Sasa, najua Ndugu Branham yupo hapa.” Kasema, “Kama akitaka kuruhusu kusanyiko liondoke, vema,” kasema, “ukitaka.” Alijua mahali nilipokuwa, kwa hiyo, alikuwa ameniona. Kwa hiyo nikasema... Mimi... Yeye... Nami nikaketi tu kimya. Na kwa hiyo, akasema, “Ndugu Branham, najua unanisikiliza, kama unataka kuja,” basi kila mtu alikuwa akiangalia huku na huku, kasema, “ukitaka kuja,” kasema, “unaweza kuja na kuliruhusu kusanyiko lifumukane.” Nami nikaketi tu kimya.

Na baada ya kitambo kidogo mimi... huku ndugu yangu ameketi pale, akasema, “Kaa kimya.”

Nikasema, “Hivi sijakaa kimya?”

⁶³ Kwa hiyo basi, yapata tu wakati huo, nikasikia *Kitu fulani*, nikaangalia juu, na kulikuwa na ile Nuru ikining’inia juu yangu, nikasimama nipate kushuka.

Mke wangu, aliyeketi pale nyuma, akamwambia Howard, ndugu yangu, kasema, “Usifanye hivyo! Kaa hapo. Hiyo hapo.”

64 Kwa hiyo yapata mabawabu mia tano wakashikana mikono, na watu, watoto wachanga wakijaribu kugusa ninii yako... mnajua jinsi ilivyo, na kwa hiyo, inasikitisha. Basi tulipokuwa tukishuka kwenda jukwaani, nilisema, “Sasa, kama ni maono yanayoshukiwa, agizo langu kutoka kwa Mungu...” Nikasema, “Bw. Best alisema nilikuwa mponyaji.”

Ndipo akakimbia jukwaani, kasema, “Kama mwanadamu, ninapendezwa nawe, lakini kuhusu fundisho limeza.”

65 Nikasema, “Ninaweza kutoa pongezi zizo hizo.” Na kwa hiyo basi, tukaninii tu... Akaendelea mbele. Na—na kwa hiyo sisi... Akaketi chini. Nikasema, “Mtu yeyote asiwazie mabaya juu ya huyu mtu sasa, yeye ni Mmarekani, ana haki, hiyo ni,” Vita vya Korea vilikuwa vikiendelea wakati huo, nikasema, “yeye, huo ndio wavulana wetu wanaopigania, uhuru wa dini.” Nikasema, “Lakini kabisa hatukubaliani juu ya Maandiko. Lakini labda...”

66 Nikasema, “Nilifikiri alikuwa mwaminifu mpaka alipojaribu kuwanyang’anya watu hao pale, ambao wana... Alisema aliwasikitikia waliolala pale kwenye vitanda hivyo vya wagonjwa, na sasa anajaribu kuwaondolea tumaini pekee walilobaki nalo, madaktari wamewakatia tamaa. Na kuna mamia walioketi pale, wameponywa katika majuma mawili yaliyopita, hapa. Na hapa, watu hawa, akijaribu kuwanyang’anya tumaini pekee walilo nalo, kufanya namna fulani ya fundisho la kishenzi, lililovurugika kuwa ni kweli.” Nikasema, “Sidhani yeye ni mwaminifu, asingeweza kuwa, katika kufanya hivyo.”

67 Kwa hiyo basi nikasema, “Lakini mimi nanena, mimi ni mwanadamu tu, lakini lile agizo, Mungu atathibitisha hilo.” Mara niliposema hivyo, Hii hapa ikaja, ikizunguka-zunguka chini namna *hiyo*. Watu wakaanza kuzimia, kupiga mayowe, na kadhalika. Wakaipiga picha.

68 Bw. Ayers, yule aliyeipiga alikuwa ni Mkatoliki, linaonekana la ajabu, lakini alikuwa akifanya kazi na mtu mmoja, Myahudi, jina lake Kipperman. Basi walipoona... Alichukua moja kule, na kutia asidi, na kuichunguza, akatoa negativu, na kila moja ya hizo picha za Bw. Best akitikisa ngumi yake chini ya pua ya mzee huyo mtakatifu, kila moja yazo ilikuwa tupu, haikupiga hata kidogo, Mungu asingeruhusu zipigwe, lakini walipoipiga hiyo picha, huyo hapo Malaika wa Bwana amesimama pale.

69 Waliichukua hapo awali, wapate kuituma hapa Washington, DC, na kuifanyia hatimiliki, wakairudisha, kisha wakampigia simu George J. Lacy, yeye ndiye mkuu wa FBI wa alama za vidole pamoja na hati. Nao wakaichukua na kuichunguza kwa yapata siku tano, ndipo tukakutana katika jengo la Houston Shell kule.

Na—na kwa hiyo wakasema, “Ni nani jina lake Branham?”

Nami nikamwambia ni langu, kisha nikasimama.

Kasema, “Utaondokea maisha haya kama watu wote.”

Nikasema, “Mimi . . . Ninajua hilo.”

⁷⁰ “Lakini,” kasema, “maadamu kuna ustaarabu wa Kikristo, picha hii haitakufa kamwe.” Akasema, “Imesemwa na mnafiki wa kale,” alimaanisha asiyeamini, akasema, “kwamba mambo ya kimbinguni kamwe yasingeweza kuthibitishwa kisayansi.” Akasema, “Bw. Branham, nilisema ilikuwa ni saikolojia, kwamba ulikuwa ukiyasoma mawazo ya watu,” akasema, “Lakini, Bw. Branham, jicho la kimitambo la kamera hiyo halitapiga picha saikolojia, Nuru iliigusa lenzi.” Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo, imepigwa picha mara nyingi, nyingi tangu wakati huo.

⁷¹ Asili Yake ni nini? Ni Yesu. Angalieni, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo alikuwa ndiye yule Malaika wa Agano, ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli? Kama unaamini Biblia! Akasema, “Mimi ndimi MIMI NIKO.” Ili kwamba, Yeye alikuwa ndiye MIMI NIKO.

⁷² Sasa angalieni, Yeye alikuwa duniani, Naye akasema, “Nilitoka kwa Mungu, Nami narudi kwa Mungu.” Hiyo ni kweli? “Nimetoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu.”

⁷³ Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka . . . Sasa, angalieni kile Nuru hiyo ilichofanya wakati ilipokuwa ndani ya Yesu, ile ishara, jinsi alivyoangalia nje, akayatambua mawazo yao, na kuwaambia walikuwa nani, na nini, na kadhalika, akithibitisha Yeye alikuwa ndiye Masihi. Sasa, wakati hiyo, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Yeye alirudi kwa Mungu Baba, naye Paulo, akienda zake Dameski, Nuru kubwa ilimulika na kumpofusha. Hiyo ni kweli? Ndipo akasema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.” Hiyo ni kweli? Alienda kwa Mungu; alitoka kwa Mungu, na akaenda kwa Mungu.

⁷⁴ Petro, gerezani usiku huo, Nuru hiyo iliingia gerezani, ikafungua milango mbele yake, Malaika wa Bwana; na huyo daima ni Yesu Kristo, Malaika wa Agano, bila shaka.

⁷⁵ Na sasa, leo hii, kama imesharudi . . . Kwa mara ya kwanza katika historia yote ya upigaji picha na ikapigwa. Ujerumani iliuliza kama wangeweza kuipiga.

⁷⁶ Nikasema, “Labda.” Wengi wenu ninyi nyote, labda, mmeiona hiyo ikija, ambapo Ujerumani ilikuwa imeweka ile kamera kubwa, na kupiga picha, ikishuka wakati ilipokuwa ikitia mafuta, kile ilipokuwa ikimwambia huyo jamaa, nilikuwa nikizungumza naye, na halafu ilipoondoka ikarudi.

⁷⁷ Waliipiga picha California hapa majuma machache yaliyopita, iliyo bora sana mliyopata kuona.

⁷⁸ Ni kitu gani? Inathibitisha ya kwamba Mungu yuyo huyo yuko pamoja na Kanisa Lake leo hii, akiishi miongoni mwetu, akileta Uhai ule ule uliokuwamo ndani ya Kristo uko ndani ya Kanisa. Amina. Ningeweza kuingia kwenye ninii yangu... kutoka kwenye mahubiri yangu sasa, sivyo?

⁷⁹ *Yehova-Yire*, hebu na tuchukue hili. Hili amepewa Ibrahimu. Nami kwa namna fulani nitagusia sehemu zake muhimu ili tuweze kutoka hapa ifikapo saa kumi, ikiwezekana sasa. Na sasa, ninawatakeni msikilize kwa makini, mnisikilize kwa makini.

⁸⁰ *Yehova-yire*, “Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu.” Hebu turudi nyuma na tumwingilie Ibrahimu kidogo; Ibrahimu ndiye aliyepewa ahadi. Nasi tunaweza tu kuokolewa tunapofanyika Uzao wa Ibrahimu, maana Ibrahimu na Uzao wake ndio waliopewa ahadi. Hiyo ni kweli, ndugu? Ibrahimu na Uzao wake baada yake.

⁸¹ Sasa, hebu turudi kwenye Mwanzo 12, ninaona baadhi yenu mkiliandika, Mwanzo 12, tu—tunakutana na Ibrahimu kwa mara ya kwanza. Ndipo Mungu akamwita Ibrahimu, alikuwa ni mtu wa kawaida tu, aliyeshuka kutoka—kutoka kwenye mnara wa Babeli pamoja na baba yake, na kukaa katika mji wa Wakaldayo, katika nchi—nchi ya Wakaldayo, mji wa Uru kwenye nyanda, labda aliishi maisha ya kawaida.

⁸² Naye alikuwa mtu mwenye umri wa miaka sitini na mitano kabla Mungu, ama, umri wa miaka sabini na mitano kabla Mungu hajanena naye. Sasa, hilo linatupa sisi wazee ujasiri kidogo, sivyo? Sabini na mitano, naye Sara alikuwa dada yake wa kambo, naye alikuwa amemwoa alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na minane, nao hawakuwa na watoto. Alikuwa tasa, mume alikuwa mgumba, kwa hiyo hawakuwa na watoto.

⁸³ Naye alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano, naye mume alikuwa na sabini na mitano. Sasa, kwenye umri wa miaka sitini na mitano atakuwa amekoma hedhi kwa yapata miaka kumi na mitano. Kwa hiyo, alikuwa—alikuwa tasa, naye mume alikuwa mgumba. Ndipo wao, hapakuwapo na njia kwao kupata watoto, bali Mungu alikutana naye, na kumwambia, na kumbariki, na kumpa lile agano, na kumwambia ya kwamba atapata mtoto kwa Sara, na kupitia kwa mtoto huyo angebariki mataifa yote, kupitia uzao wake.

⁸⁴ Sasa, kama ukiangalia, sasa, itanibidi nianze kufundisha kidogo hapa sasa, lakini simaanishi kufanya hivyo kwa ajili ya ubishi, lakini kama utaangalia ya kwamba hilo agano lilitolewa kwa Ibrahimu na Uzao wake. Sasa, si *wazao*, bali *Uzao* wa Ibrahimu, Uzao wa Ibrahimu. Nayo Maandiko yanasema, “Sisi tulio ndani ya Kristo tu Uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi pamoja naye sawasawa na ile ahadi.”

⁸⁵ Sasa, unafanyikaje Uzao wa Ibrahimu? Unapomchukua Kristo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, hiyo ndiyo njia pekee unayoweza kuwa Uzao wa Ibrahimu, maana hiyo hupanda ndani yako imani aliyokuwa nayo Ibrahimu.

⁸⁶ Sasa, Ibrahimu, watu wengi wanafikiri alikuwa Myahudi, hakuwa, alikuwa Mmataifa. Lakini sasa, lakini Ibrahimu na, hebu tuseme pamoja, "Ibrahimu na Uzao wake." Agano lilifanywa pamoja nao.

⁸⁷ Ibrahimu na Uzao wake, kwa hiyo hebu tuseme, "Sisi ni Uzao wa Ibrahimu." Ni wangapi walio katika Kristo? Inua mkono wako. Basi kulingana na Kitabu hiki kilichobarikiwa ninyi ni Uzao wa Ibrahimu, nanyi ni warithi pamoja, nawe ni mrithi pamoja na Ibrahimu wa mali zote ambazo Mungu aliwapa hao watu. Wewe ni Uzao wa Ibrahimu, basi huna budi kuwa na imani ya Ibrahimu kusudi uwe Uzao wa Ibrahimu. Mnalipata? Loo, natumaini hivyo.

⁸⁸ Angalieni sasa, agano lilifanywa kwa Ibrahimu bila masharti. Sasa, Yeye alifanya agano na Adamu, "Kama utafanya jambo fulani, nitafanya jambo fulani." Basi mwanadamu daima huvunja ahadi yake kwa Mungu, agano lake, daima. Lakini agano hili, mnaliona? Lilikuwa ni kwa Ibrahimu na Uzao wake bila masharti. Sio, "Ukifanya." "Nimefanya!" Mnaona hilo? Kwa Uzao wa Ibrahimu, si kwa ulimwengu wa nje sasa, kwa Ibrahimu na Uzao wake hilo agano lilikuwa bila masharti. Si, "Ukifanya, nitafanya," bali, "Nimefanya tayari, kwa ajili yako."

⁸⁹ Kwa hiyo "Lithibitishe alasiri ya leo," si lazima Mungu ashuke aje na kufanya upasuaji mwingine upate kuponywa, amekuponya tayari. *Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*. Umeponywa tayari, jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuupokea tu. Usiponyosha mkono na kuuchukua, wewe ni Uzao wa Ibrahimu, basi unaamini, na tayari upo. Kwa hiyo, hakuna—hakuna kuutilia shaka, tayari upo, ni wako. Loo, jamani! Laiti ningaliweza...laiti hilo lingeweza kulipua moto, kama tu kumimina, kurusha kiberiti kwenye baruti.

⁹⁰ Angalieni, mnaona ninalomaanisha? Tayari ni wako, ni mali yako, kwa kuwa wewe ni Uzao wa Ibrahimu kama umempokea Roho Mtakatifu. Umetiwa muhuri, umekufa, na uhai wako umefichwa katika Kristo kwa njia ya Mungu, umetiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu. Muda gani? Mpaka uamsho ujao? Hata siku ya ukombozi wako. Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu."

⁹¹ Kabla behewa halijatiwa muhuri, behewa, kila kitu hakina budi kuingia mle ndani vizuri kabisa, hiyo ndiyo sababu wengi sana hawampokei Roho Mtakatifu, walegevu kupindukia. Kama vile tai akiwapandisha watoto wake juu, yeye huyapeperushia

manyoya yote yaliyolegea yakatoka mle, kabla hajafika huko juu, la sivyo angevunja shingo yake. Mnaona?

⁹² Halafu, kunguru kamwe asingeruka pamoja na tai. Mungu huwafananisha manabii Wake na tai; Yeye Mwenyewe ni tai. Kunguru asingeweza kamwe kuruka, kumfuata tai. Loo, kama mwewe angejaribu, angesambaratika hewani. Vema, hakika, tai ni ndege aliyeumbwa maalum, kwa hiyo hana budi kuwa na manyoya maalum, na macho maalum ya kupanda juu, juu sana, juu sana juu ya kitu chochote kile. Hivyo ndivyo watu wa Mungu wafanyavyo, makinda wa tai wa Mungu, wanapanda juu, nao wanajua wao ni Uzao wa Ibrahimu, wanaamini chochote, haidhuru hali ya mambo ikoje, wako mbali na dunia, wako juu sana katika angahewa.

Loo, niinue juu ya vivuli,
Nipe ushirika pamoja Nawe; (Hiyo ni kweli.)

Ipandishe miguu yangu mahali pa juu.

Nipandishe, Bwana, jalia nisimame,
Kwa imani, kwenye nchi ya meza ya Mbinguni.
Kiwango cha juu kuliko nilichopata;
Bwana, inua miguu yangu mahali pa juu zaidi.
(Juu kabisa.)

⁹³ Ibrahimu na Uzao wake baada yake, agano hilo halikuwa na masharti kabisa kwa Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Sasa, hilo ni zuri sana.

⁹⁴ Sasa, ninii, Ibrahimu alifanya nini? Ibrahimu alimwamini Mungu. Sasa, Yeye atafanyaje jambo hilo, naye ni...? Sasa yeye ana umri wa miaka sabini na mitano, basi atampataje mtoto huyu kwa ninii yake...? Mke wake sasa ana umri wa miaka sitini na mitano. Na ungeweza kuwazia, mume na mke wazee kama hao wakishuka kwenda kwa daktari na kusema, “Daktari, nataka utengeneze chumba hospitalini, mke wangu atapata mtoto?”

“Una umri gani, bwana?”

“Nina sabini na mitano.”

“Mke ana umri gani?”

“Sitini na mitano.”

“Maskini jamaa mzee.” Mnaona?

⁹⁵ Vema, mtu yeyote anayemwamini Mungu kwa Neno Lake, watasema jambo lile lile kukuhusu. “Kwa maana wote wanaoishi maisha ya kitauwa katika Kristo Yesu watateswa,” Yesu alisema hivyo. Sasa, unaeleweka vibaya kwa sababu hawa ni Mmarekani, Mjerumani, Uswisi, bali wewe umetoka Mbinguni. Umezaliwa kutoka huko juu, kwa hiyo unaamini yale Mungu aliyosema.

⁹⁶ Sasa, angalieni jambo hili: Ungeweza kuwazia hao mume na mke wazee, ninaporudia tena katika kusema, Ibrahimu alisema, “Sara,” baada ya zile siku ishirini na nane za kwanza, mnajua, “unajisikiaje, Mpenzi?”

“Mpenzi, hakuna tofauti hata kidogo.”

⁹⁷ “Utukufu kwa Mungu, tutampata haidhuru.” Hiyo ni kweli. “Weka tayari vijibuti, chukua jicho-ndege, na pini, na uandae kila kitu, tutampata.”

“Unajua? Ibrahimu, unamaanisha nini kwa hilo?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha, hilo—hilo tu ndilo ninalohitaji kujua. Mungu alisema hivyo.”

Vema, mwaka mmoja ukapita, “Mpenzi, chochote tofauti?”

“Hata kidogo.”

“Utukufu kwa Mungu, ni mwujiza mkubwa zaidi sasa, ni mwaka mmoja baadaye.”

⁹⁸ Baada ya kitambo kidogo, miaka ishirini na mitano ikapita; Biblia ilisema alipata nguvu zaidi na zaidi. Nasi tunasema ati sisi ni Uzao wa Ibrahimu, tunaombewa, na kesho yake, “Unajisikiaje?”

“Sininii, nadhani sikuupata, sijisikii vizuri zaidi.” Ati Uzao wa Ibrahimu! Loo, jamani! Mnaona ninalomaanisha? Uzao wa Ibrahimu ni haba.

⁹⁹ Uzao wa Ibrahimu, sasa, hebu tusikiri kitu fulani isipokuwa tumekimiliki kweli, mnaona, Uzao wa Ibrahimu. Wakati Uzao wa Ibrahimu unapoishika ahadi ya Mungu, itadumu, haidhuru ni kitu gani kinachotukia, hakuna kitu kitakachowatikisa kamwe. Na inapokawia, wanapata nguvu zaidi.

¹⁰⁰ Naye akaendelea kumpa Mungu sifa wakati wote. Baada ya miaka ishirini na mitano, sasa yeye ana umri wa miaka mia moja, naye mke ana tisini, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Lakini utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile. Pangusa tu mavumbi kwenye vijibuti na kadhalika, na kila kitu, anakuja.”

“Unajua? ”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mungu aliniambia hivyo, ni hayo tu.”

¹⁰¹ Sasa, hivyo ndivyo Uzao wa Ibrahimu ulivyo. Kama ninyi ni warithi wa Ibrahimu, mna imani ya namna hiyo. Je, ninyi ni Uzao wa Ibrahimu? Hebu tuseme, “Amina.” Hakika, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, bila shaka, ndivyo tulivyo. Mungu asaidie kutokuamini kwetu. Hiyo ni kweli.

¹⁰² Sasa, kila kitu kiko tayari, tukijiandaa kwa ajili yake. Sasa, hiyo ilikuwa katika mlango wa 12 wa Mwanzo. Sasa, katika

mlango wa 15 wa Mwanzo Mungu alithibitisha agano hili pamoja naye. Sasa, ni yapata miaka mingi baadaye, kwa hiyo siku moja Mungu alikuwa akizungumza na Ibrahimu, Naye akasema, “Ibrahimu, nitathibitisha jambo hili, nita—nitakupa ishara.” Mungu daima hutoa ishara.

¹⁰³ “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, watapeana mikono na mchungaji, na kuweka jina lao kwenye kitabu.” Huenda hilo likawa katika shajara ya mwaka, bali si katika Biblia. Mnaona? Hiyo ni kweli. Naam.

¹⁰⁴ “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, wakishika nyoka, au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ishara hizi zitafuatana na waaminio.

¹⁰⁵ Kwamba, mikono ikiwekwa juu ya mwaminio huyo, mwaminio huyo anasema, “Amina! Mimi ni Uzao wa Ibrahimu. Ninaliamini.” Ndipo yeye, anafanya kazi vizuri, inatimia. Sasa, ishara hizi . . .

Ndipo Ibrahimu akamwambia Mungu, “Nitajuaje jambo hili?”

Akasema, “Ibrahimu, nenda uniletee mbuzi jike, na ndama, na kondoo dume, utoe dhabihu.”

¹⁰⁶ Ndipo Ibrahimu akawakata vipande, akawachinja, akawatenganisha, akachukua hua na njiwa mdogo, na kuwatupa ndani, na kufanya—na ku—kumtolea Bwana dhabihu. Basi alipofanya hivyo, alingojea hapo, na kuwafukuza ndege kutoka kwe—kwenye hicho chakula mpaka jua lilipokuwa linatua, ndipo wakati jua lilipokuwa likitua, usingizi mzito ukamjia Ibrahimu.

¹⁰⁷ Usingizi huo ni ule usingizi wa Milele, tulinena habari zake, watu wote hawana budi kufa. Na hofu ya kutisha ya giza mbele zake, ambapo, tanuru inayotoa moshi, ambapo . . . Kila mtu aliyezaliwa katika ulimwengu huu huja ulimwenguni ameumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo, mwongo, mwovu, aliyekataliwa, mara tu anapozaliwa.

¹⁰⁸ Kwa hiyo hatuninii, tunazaliwa, hata hatuna nafasi na, nje ya Damu ya Yesu Kristo. Halafu basi, kila mmoja wetu tunaistahili hiyo kuzimu. Lakini mbali na hayo ilitokea Nuru ndogo nyeupe, iliyoingia katikati ya vipande hivi vilivyogawanyika vya dhabihu.

¹⁰⁹ Sasa, kama tungalikuwa na wakati, ningetaka kuwaambia kile kila mmoja wa hao aliwakilisha, mbuzi jike, na kondoo dume, na ndama. Basi mliona, yeye hakuwakata hao hua wawili? Wanawakilisha uponyaji wa Kiungu, mnaona. Kwa hiyo, kamwe hakuwakata, kamwe hakuwapasua vipande.

¹¹⁰ Lakini wakati Nuru hii ndogo ilipoingia katikati ya hizo, hizo mbili, Yeye alikuwa akimthibitishia Ibrahimu lile agano, yale angefanya naye pamoja na Uzao wake, na jinsi huo Uzao ungekuja, na jinsi angetimiza ahadi Yake; ulikuwa ni mkataba ukitiwa sahihi. Sasa, Yeye alimaanisha nini?

¹¹¹ Sasa, hebu tuchukue hapa Marekani, kama ningesema ya kwamba—ya kwamba Ndugu hapa, mimi na mmoja wa hawa ndugu tulikuwa tukitaka kufanya m—mkataba ama mapatano, agano ni mapatano, kama tungefanya agano sisi kwa sisi, tungeketi chini na kulizungumzia sisi kwa sisi, labda tuandike mkataba wetu, chochote ulichokuwa, tule pamoja, nasi tungepeana mikono, tuseme, “Uweke *hapa*. Tu—tu—tunakubaliana kufanya jambo hili.” Hilo ni agano huku Marekani.

¹¹² Sasa, kama tulikuwa huko Japani, agano huko Japani, wanafanya mapatano, halafu wanachota chumvi kidogo na kurushiana chumvi. Hiyo ni desturi ya huko Japani, kufanya agano.

¹¹³ Lakini katika siku za Ibrahimu huko mashariki, jinsi walivyofanya agano, walikata, walimwua mnyama, na kumpasua vipande, kisha wakaandika mapatano yao juu ya ngozi hii—hii, ama, ngozi yao ya mwana-kondoo, kisha wanasimama mle ndani na kula kiapo kwa dhahibu hii ya mnyama aliyekufa, kama mmoja akilivunja, mwili wao na uwe kama mwili wa mnyama huyo uliovunjwa. Halafu wanauvunjavunja huu, mtu mmoja anachukua kipande kimoja, na mmoja kingine. Na mahali maandishi hayo yalipokuwa, kamwe hayawezi kuunganishwa, isipokuwa kipande kiki hiki kirudi kuyaunganisha tena. Kwa sababu wakati kinaporaruliwa, kinapasuka huku na huko, na kadhalika, ngozi hiyo ya mwana-kondoo inaporaruliwa, mahali yalipo hayo maandishi.

¹¹⁴ Ndipo wanakihifadhi hicho, na ndipo njia pekee ambayo agano hili linawekwa ni wakati, litakapotimia ni wakati wanaporudi, kila kipande cha karatasi hii ya ngozi hakina budi kuungana pamoja, kuunganishwa kikamilifu kufanya mapatano yale yale hasa.

Sasa, mnasema, “Mungu alikuwa akifanya nini pale basi, Ndugu Branham?”

¹¹⁵ Haya hapa yale aliyokuwa akionyesha kupitia Uzao wa Ibrahimu: Ibrahimu alisema, “Ninaenda zangu hali sina mtoto,” mlango wa 15 wa Mwanzo, “na mimi sina mrithi, na huyo ni huyu Eliezeri wa Dameski.”

¹¹⁶ Akasema, “Haitakuwa ni yeye. Lakini lile agano, yule ninayefanya agano naye, anatoka ndani ya viuno vyako mwenyewe. Itakuwa ni kupitia kwako na Sara,” kwa maneno mengine, “ndilo nitakalofanya.” Na sasa kumbukeni, yeye ni mzee sana.

117 Sasa, Yeye alikuwa akionyesha nini? Kwamba kupitia kwa Ibrahimu alikuja yule aliyeahidiwa, Isaka; na kupitia Isaka akaja Yesu. Na kupitia kwa Yesu, Isaka alikuwa tu baba wa Israeli, bali kupitia kwa Yesu yeye ni baba wa kila taifa, Uzao wote wa Ibrahimu. Naye alilithibitishaje? Akionyesha yale angefanya kwa dhabihu.

118 Sasa, Yesu alifanyika Dhabihu hiyo. Naye akaenda Kalvari, ndipo Mungu akamrarua vipande viwili pale Kalvari, akararua Nafsi Yake na Roho kutoka mwilini Mwake, kisha akaufufua mwili Wake katika siku ya tatu, na kuuweka kwenye mkono Wake Mwenyewe wa kuume, kisha akamtuma Roho yeye yule aliyekuwa juu Yake kufanya kazi katika Kanisa Lake apate kuuza Uzao wa Ibrahimu. Hivi hamwezi kuliona, ni ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hilo ndilo thibitisho, linalolithibitisha.

119 Sasa, kanisa linalokiri kuwa ni kanisa la Kikristo, italibidi kuwa na Roho yuyo huyo aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo, kwa ajili ya ufufuo wa Kanisa, Kristo na Bibi-arusi Wake watakuja pamoja na kuungana kikamilifu, maandiko na ahadi za Mungu zititimiziwa pale. Kwa hiyo kuungana hakuwezekani isipokuwa Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Kristo yuko ndani yangu na yako. Na basi kama Roho yuyo huyo yuko mle ndani, atafanya kazi zile zile, na kuishi maisha yale yale yaliyotengwa, na kufanya kazi zile alizofanya Yeye. Biblia ilisema hivyo, imethibitika kote kote mpaka Mwanzo, Mwanzo ndio mlango wa mbegu. *Mwanzo* maana yake ni “chanzo.” Hapa linathibitisha.

120 Hilo si lingetufurahisha sisi sote? Hilo si lingemfanya mwenye dhambi...? Linapaswa kuwa la kushangaza. Linapaswa kumfanya mfuasi wa kanisa aje kwa Kristo na kukaa mpaka amejazwa na Roho Mtakatifu. Ndiyo ahadi pekee ya Kunyakuliwa, njia pekee ambayo Kanisa na Kristo wanaweza kuja pamoja, Roho mwenyewe.

121 Wakati Mungu alipomwamba mtu Wake wa kwanza katika bustani ya Edeni, hivi mliona, Yeye alimwamba mwanamume na mwanamke pia? Alikuwa mwanamume, aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, Roho, alimweka katika mwili, Mwanzo mlango unaofuata, akiisha kumwamba, mwanamume na mwanamke. Na bado hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi, kwa hiyo basi Yeye akamwamba mtu kutoka katika mavumbi ya nchi, si kwa mfano Wake.

122 Lakini basi Mungu akashuka katika mfano wa mwanadamu kwa Yesu Kristo, apate kumkomboa mwanadamu, aliyeanguka, kwa mfano wa ardhi, Naye alifanywa kwa mfano wa ardhi. Ee Mungu! Hivi hamwezi kuona Injili inamaanisha nini? Wakati Mungu alipofanyika mwanadamu ili mwanadamu awe Mungu, sisi ni wana na binti za Mungu.

123 Sasa, mtu huyu wa kwanza, Adamu, hebu mwangalieni, katika roho alikuwa wa kike na wa kiume pia. Ndipo basi

akafanyika mwili, wala hakuwa na msaidizi. Ndipo Mungu... Mwanamke hayuko katika uumbaji wa asili wa Mungu, yeye ni zao-toka la mwanamume. Kwa hiyo, kuwafanya mmoja, kuonyesha yale Yeye aliyofanya, alifungua ubavu wa Adamu, na kuchukua sehemu ya mwili wa Adamu, ili kwamba wasitenganishwe, wangekuwa mmoja, na kuchukua sehemu ya roho ya Adamu, sehemu ya mwili wa Adamu, akatoa roho ya kike kutoka kwa Adamu na kumfanya Hawa.

¹²⁴ Basi unapomwona mwanamke, jinsi baadhi ya wanawake wetu wa kisasa, kukata nywele kama wanaume, kuvuta sigara kama wanaume, kulaani kama wanaume, ukimwona mwanamke anayetaka kuwa wa kiume, kuna upotovu pale, mahali fulani. Ndipo unapomwona mwanamume amekuwa dondoadume na ninii, anaonekana kama bata ameketi kichalichali, na kadhalika namna hiyo, na anataka kuvaa nguo za wanawake wakati wote, kuna kitu kilichopotoshwa pale, mahali fulani. Mungu aliwaumba wanaume kuwa wanaume, na wanawake kuwa wanawake. Biblia ilisema...

¹²⁵ Siku moja nilikuwa nikizungumza dhidi ya wanawake kuvaa kaptura, ndipo mwanamke mmoja akaniambia, "Sizivai."

Nikasema, "Ni kitu gani hicho umevaa?"

Akasema...Vitu hivyo ni nini? Visukuma pedali, ama chochote kile, namna hiyo. Nikasema...La, suruali ya dangirizi.

Nikasema, "Ni...Hilo ni baya kuliko hapo awali! Biblia ilisema ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi limpasalo mwanamume." Kweli.

¹²⁶ Huko Klamath Falls, hivi majuzi, mama mmoja aliniandikia barua kubwa, ndefu, akasema, "Vipi kuhusu mwanamke, basi, huko nje amepanda farasi katika eneo lililojaa mbu, huko nje akiendesha, akiwakusanya ng'ombe? Unaonaje kuhusu yeye kuvaa nguo ya kike huko nje? Ama wakati akiwa bustanini, wakati inambidi kuinama na kung'oa vitu kutoka bustanini?"

¹²⁷ Nikasema, "Mama yangu na mke wangu wote wawili wanavaa nguo, wala hawana shida nazo. Wanazivaa ndefu vya kutosha wanapoinama chini, hivyo tu." Halafu nikasema, "Jambo lingine, juu ya, huko nje juu ya farasi, kupanda farasi, mwanamke hana shughuli yoyote huko nje."

¹²⁸ Hayo ndiyo maangamizi ya taifa letu siku hizi, ni wanawake kujaribu kuchukua kazi za wanaume. Yeye anajaribu kuwa mwanamume, huku mwanamume akitaka kuwa mwanamke, Mungu aliwafanya tofauti. Kweli. Hana shughuli kuwa hivyo, ametoka kwenye kitengo chake, na mwanamume yuko nje ya kitengo chake. Loo, jamani! Isimamisheni, saa!

¹²⁹ Angalieni, Mungu aliwafanya tofauti. Naye akafanya agano na Adamu, akafanya agano na Hawa. Lakini mnaona, Yeye

aliwafanya mmoja, wao si wawili tena, bali ni mmoja. Sasa, vivyo hivyo Kanisa na Kristo.

¹³⁰ Mungu kamwe hakusema nendeni mkafaye dhehebu linaloitwa *Hivi-na-hivi*, ama mwende mkawaelimishe *hivi*, alimchukua Mwanawe Mwenyewe, na kutoka moyoni Mwake, vitu vitatu vikatoka katika mwili Wake. Samahani, akina dada, ninataka kutoa wazo muhimu. Katika kuzaliwa kwa kawaida, jambo la kwanza linalotukia katika kuzaliwa kwa kawaida ni lipi? Maji. Halafu, damu. Ni kitu gani kinachofuata? Uhai. Hicho ndicho kitu kile kile kinafanyiza kuzaliwa upya. Ni kitu gani kilichotoka ubavuni mwa Yesu? Maji, Damu, na “Mikononi Mwako naiweka Roho Yangu.”

Yohana Mtakatifu, ama, Yohana wa Kwanza 5:7 ilisema:

...wako watatu washuhudiaao mbinguni, Baba, Neno, (Ambalo ni Mwana.) na Roho Mtakatifu: ...watatu hawa ni mmoja.

¹³¹ Huwezi kuwa na Baba pasipo kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu, “Hawa watatu ni Mmoja.”

Na wako watatu washuhudiaao duniani, maji, damu, na Roho: wao si mmoja, bali wanapatana kwa habari moja.

¹³² Unaweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa, unaweza kutakaswa bila kumpokea Roho Mtakatifu. Mnaona ninalomaanisha? Luther alihubiri kuhesabiwa haki, Wesley alikuwa na utakaso, Pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ni kama tu mbegu iliyopandwa: ubua, kishada, suke, kila kitu ulimwenguni ni mfano wake. Kweli.

¹³³ Sasa, Mungu alimpasua Kristo vipande viwili, akamtuma Roho Wake, anayeitwa Roho Mtakatifu, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni Mimi tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi,” *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari,” si chini tu kwa ajili ya wakati fulani, bali hata mwisho wa ulimwengu.

¹³⁴ “Enendeni ulimwenguni kote.” Ishara hizi zitafuata kwa muda gani? Ulimwengu wote, Marko 16, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Halijawahi kutukia bado. Ishara hizi zitafuata kwa muda gani? Mpaka itakapokwisha. “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili, kila kiumbe. Ishara hizi zitafuatana na viumbe hao waaminio.” Mnalipata?

¹³⁵ Sasa angalieni, hiyo ilikuwa ni mlango wa 15, sasa hebu twendeni kwenye mlango wa 17. Sasa, Mungu alimtokea Ibrahimu katika Jina jingine, Mlango wa 17 Yeye alimtokea katika Jina la *El Shaddai* neno la Kiebrania, Mungu Mwenyezi, *El Shaddai*. Sasa, *shad*, linamaanisha “titi” kama mama, mwanamke; *shaddai* ni katika wingi, “mwenye matiti.”

¹³⁶ Sasa, Yeye alikuwa akifanya nini na Ibrahimu hapa? Sasa, Yeye alikuwa amempa agano katika Mwanzo 12, bila masharti; Mwanzo 15, Yeye akamthibitishia, yale atakayofanya, na jinsi atakavyoyafanya; sasa katika Mwanzo 17 Ibrahimu sasa ana umri wa miaka tisini na tisa, moja kwa moja kwenye mia moja, hiyo ingemfanya Sara awe na themanini na tisa.

¹³⁷ Sasa, Biblia ilisema ya kwamba mwili wake ulikuwa kama uliokufa; tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Lakini Yeye alimtokea katika Jina la *El-Shaddai*, “Mwenye matiti,” kiasi cha kusema, “Ibrahimu, Mimi ni Mungu mwenye matiti,” si *titi*, *mwenye matiti*, mawili. “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa,” Agano Jipya na la Kale.

¹³⁸ Kwa maneno mengine, wakati mtoto mchanga anapohangaika na kuugua, mama humchukua jamaa huyo mdogo na kumweka kwenye titi lake, ndipo huyo mtoto mchanga ananyonya nguvu zake kutoka kwa mama.

¹³⁹ “Na karibu, Ibrahimu wewe ni mzee, una umri wa miaka mia moja, na nguvu zako zimekwisha, bali Mimi Ndimi niliyetoa ahadi, Mimi ni Titi lako, egemea tu kwenye ahadi Yangu na uendelee kunyonya.”

¹⁴⁰ Na jambo lingine, mtoto mchanga ameridhika mradi tu anamnyonya mamaye, maskini jamaa huyo hahangaiki tena, mara anapoanza kumnyonya mama yake, ameridhika. Na Yeye ndiye Mridhishaji, Mwenye nguvu, Mlishaji, Mpaji nguvu. Maskini mtoto mchanga akilalia titi la mama yake, ameridhika, ananyonya arejeshe nguvu na afya tena. Sasa, hiyo ni kwa Ibrahimu na kwa Uzao wake.

¹⁴¹ Sasa, kama wewe ni mgonjwa leo, naye daktari anasema, “Dada, nachukia kukwambia, una ugonjwa wa moyo, moyo wa—wako ni mbaya sana”:

“Ndugu, u—una kansa, hakuna chochote, sayansi yangu ya tiba inaonyesha ya kwamba ha—hatuwezi, imeendelea, hakuna kitu tunachoweza kufanya.”

¹⁴² Nawe ni Uzao wa Ibrahimu, na *Kitu Fulani* kinaendelea kukwambia, “Nina maisha zaidi ya kuishi.” Ni kitu gani? Ni Mungu akijaribu kusema, “Njoni Kwangu, ninyi ni Uzao wa Ibrahimu, Mimi ndimi ninayewapa nguvu zenu, Mimi ndimi Mridhishaji wenu.”

“Itachukua muda gani?”

¹⁴³ Vema, vipi kama mtoto huyo ataliacha titi la mama yake wala hatanyonya tena? Atakufa. Basi tunapomchukua Mungu kama Mponyaji wetu na kisha tuseme, “Loo, vema, labda nilikosea,” la, watoto wa Ibrahimu hawafanyi hivyo, wanaishikilia ahadi hiyo moja kwa moja, na kuinyonya. Kama ni wokovu, Roho Mtakatifu, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu.” Kama ni uponyaji

wa mwili, “kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Yeye ni Mungu mwenye matiti.

¹⁴⁴ Ni ninii...! Yeye, Yeye alikuwa akifanya nini? Alikuwa akimweka Ibrahimu katika hali ya kupokea ule mwujiza uliokuwa karibu kutukia.

¹⁴⁵ Sasa, fungua ukurasa mwingine wa Mwanzo 18. Sasa, tunaona katika Mwanzo 18 alipewa ishara kuu. Sasa kumbukeni, Mungu alimwambia Ibrahimu katika Mwanzo 12, pia, ajitenge na watu wake wote, jamaa yake yote, na kukaa pamoja Naye kama mgeni katika nchi ya kigeni.

¹⁴⁶ Sasa, Mungu anataka watenganishaji; sasa, watu wanataka wachanganyaji. Loo, jamani! Siku hizi hawana budi kuwa na maskini jamaa mdogo wa Hollywood, mwajua, na—na, mwajua, *haya* yote, na hapana budi kuwe na maua mengi, na kupakwa rangi tu. Hawamtaki mhubiri wa mtindo wa kale anayekemea mambo, hawatakubali, “Yeye ni mlokole, yeye ni mtakatifu anayejibingirisha.” Hilo ndilo wanalotaka, wanataka wachanganyaji, mtu atakayeenda kuogelea pamoja nao, na mtu atakayecheza karata pamoja nao, na mtu atakayeenda kwenye madansi, wala si mlokole, mnaona, hawamtaki huyo. Lakini Mungu anataka watenganishaji.

¹⁴⁷ Jitenge! Neno lenyewe *kanisa* linamaanisha, “waliotengwa, walioitwa watoke.” “Ondokeni kati yao,” asema Mungu, “nami nitawakaribisha, msiguse vitu vyao vichafu.” Watenganishaji, loo, ewe Mkristo, jitenge na kila kitu cha ulimwengu, ndugu, dada, acheni mambo ya ulimwengu, jitengeni.

¹⁴⁸ Sasa, Ibrahimu alikuwa...Mpaka alipotii hilo kikamilifu, Mungu kamwe hakambariki, alimchukua baba yake akaenda naye, akamchukua Lutu, mpwawe. Nayo ilifanya nini? Huyo mzee alikuwa ni kisirani tupu maadamu aliambatana naye; hatimaye, akafa.

¹⁴⁹ Halafu Lutu, walikuwa wakizozana, na kupigana, wakigombania maeneo ya kuchunga mifugo, na kadhalika, mpaka Lutu alipojitenga na kushuka kwenda Sodoma. Alishika njia ya kushuka, njia rahisi, dola chache za ziada, basi mnaona ilichomgharimu? Alitaka kuwa maarufu, akawa meya wa jiji hilo. Kwa hiyo, alikuwa huko chini, alitaka kuwa na jina kubwa. Kuna watu wengi sana wanaotaka majina *makubwa*, mambo *makubwa*. Inahitaji tumbili kurukia vitu vinavyometameta na vitu kama hivyo. Naam, bwana. Je, mliwahi kumwona tumbili? Chochote kinachong’aa atakirukia. Unaona?

¹⁵⁰ Ndipo, sasa mnaona Lutu, aliwazia, “Labda, kama nikishuka kwenda kule Sodoma nitakuwa mtu maarufu, jina langu litajulikana.” Hakika, liangalieni leo hii jinsi linavyojulikana. Naye Bibi Lutu, alifuata mbinu zote, na mitindo, na kadhalika, mwangalieni siku hizi, amesimama pale uwanjani kama nguzo ya chumvi. Naam. Lakini Sara akashika

njia pamoja na mumewe, njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, kutembea katika ushirika pamoja na Mungu, walikuwa na mahali pagumu.

¹⁵¹ Ndipo siku moja wakati Ibrahimu alipokuwa akiondoka... Nchi ilikuwa kame, wakati mwingine tunafikiri ya kwamba mambo hayo ni laana, la, kama unajua moyo wako uko sawa na Mungu, haijalishi ni jambo gani linalotukia, dumu moja kwa moja nalo. Ibrahimu na Sara, labda hali ya hewa yenye joto, na wanyama wote walikuwa wamekonda, na kadhalika, halafu siku moja Ibrahimu alikuwa ameketi chini ya mwaloni yapata adhuhuri, katika mlango wa 16, ama mlango wa 18, hasa, wa Mwanzo. Naye Mungu alikuwa amechoshwa na hiyo Sodoma na Gomora, kama vile tu Yeye alivyochoshwa na ulimwengu huu leo, amechoshwa na upumbavu wao, kwa hiyo Yeye atashuka apate kuuangamiza.

¹⁵² Kwa hiyo Yeye alikuwa anataka kuwapa ishara kwamba hiyo ilikuwa inaenda kuangamizwa. Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa ameketi pale chini ya mwaloni, naye akaangalia na kuona watu watatu wakija. Nao wakaja mahali alipokuwa, akakimbia kuwalaki, naye akasema, "Bwana wa—wangu." Sasa, mtu fulani alikuwa akijaribu kuniambia huyo alikuwa ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, mnaona. Huo ni uwongo. Kamwe hakusema, "Bwana zangu." Alisema, "Bwana wangu."

¹⁵³ Lutu baadaye aliwaita wahubiri wawili walioshuka kule, si herufi kubwa *B, b* ndogo, "Mmenijia, bwana zangu" Lutu huyo aliyerudi nyuma. Kwa hiyo, akasema, "Bwana zangu."

Lakini Ibrahimu alipokutana na hao watatu, alisema, "Bwana wangu," herufi kubwa *B-w-a-n-a*, Elohimu, Bwana. Hao watatu walikuwa wamesimama pale, lakini alisema, "Bwana wangu."

¹⁵⁴ Sasa, walipokaribia, yeye alisema, "Njoni hapa mketi chini, na—na hebu nilete maji kidogo na nioshe miguu Yako, na—na mkapumzike, na kula chakula kidogo, ndipo mngeweza kuondoka, kwa kuwa ulisimama kumwona mtumishi wako."

Vema. Walipokuja, kasema, "Basi fanya hivyo." Kwa hiyo wakaenda pale na kuketi chini.

¹⁵⁵ Ndipo Ibrahimu akaenda hemani mbio, ile hema kuu, hema kubwa alimoishi, labda watumishi wote walipiga kambi kandokando, kijiji chao. Kwa hiyo akarudi mbio kwenye hema kuu, kubwa, na akasema, "Sara, kanda vipimo vitatu vya unga, upesi sana, na uvioke mekoni." Naye a—akakimbia kwenye kundi, na kuchukua ndama aliyenona sana na kumpa mtumishi wake amwandae, akasema, "Mtayarisha, upesi sana."

¹⁵⁶ Nao wakamtayarisha, naye akatoka, na kuwalisha hawa watu watatu. Ilikuwa ni kitu gani? Nyama ya ndama, huyo ndama, aliwalisha maziwa, na mkate, na siagi, nao wote wakaketi na kula, wote. Na hata hivyo, Mmoja wao

alikuwa Yehova Mungu. Kweli. Ibrahimu alizungumza Naye. Msingeyatilia shaka Maandiko, sivyo? Yeye alisema alikuwa Elohimu, hiyo ni kweli, Mungu; alitaja yapata mara sita ama saba, papo hapo mfululizo, Elohimu, huyo Ndiye.

¹⁵⁷ Mtu mmoja aliniambia wakati mmoja, kasema, “Kweli huamini huyo alikuwa ni Mungu.”

Nikasema, “Hakika, ninaamini ni Mungu, Ibrahimu alisema Ndiye, Biblia ilisema alikuwa, nayo imani yangu imejengwa juu ya Neno la Mungu.”

Kasema, “Mungu angewezeaje kufanyika mwili?”

¹⁵⁸ Nikasema, “Kama vile alivyokuwa wakati alipokuwa katika Yesu Kristo, alifanyika mwili.” Hakika, alikuwa mwili. Wakati alipokuwa katika Melkizedeki, alifanyika mwili, bila shaka, alikuwa mwili, “Mfalme wa amani, Mfalme wa Salemu, bila baba, bila mama, hana mwanzo wa siku, wala mwisho wa miaka,” vema bila shaka, “mwisho wa maisha,” hasa. Hakika, alikuwa mwili.

¹⁵⁹ Sasa, Huyu hapa miongoni mwa Kanisa Lake leo, amefanyika mwili katika Kanisa Lake, bila shaka, Elohimu. Sasa, loo, laiti mngaliweza tu kutambua ya kwamba ninyi wanaume, mlifanywa kuwa mungu mdogo! Wewe ni mwana wa Mungu, wewe ni mrithi wa Mungu, na una milki, Mwanzo 1:26, Yeye alimpa mamlaka juu ya kila kitu duniani, Yeye alimfanya mungu juu ya nchi. Hiyo ni kweli. Yeye alimpa milki, yeye ni mfalme, mungu. Na mahali alipoangukia, angeweza kuzungumzia miti, “Geuzwa, ung’olewe ukawekwe *hapa*.” Kwa pepo na mawimbi, “Tulia,” nazo zingekomaa. Yeye alikuwa mungu, mungu mdogo, mwana wa Mungu, kama vile wewe ulivyo mwana wa baba yako.

¹⁶⁰ Na ulimwengu mzima unaugua, ukingojea kudhihirishwa kwa wana wa Mungu, ukingojea Kanisa kurudi mahali Pake tena, wana wa Mungu kudhihirishwa, ukingojea saa hiyo. Natumaini hilo haliudhi, bali ilinibidi tu kulisema. Mnaona? Kanisa liko mbali sana na mahali Pake, Linahitaji kurudi liwe wana wa Mungu tena, watawala, watawala wa dunia, chini ya utawala wa kiroho. Litarudi siku moja, wakati Yule mkuu atakapokuja, Yesu Kristo, ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu; maumbile yanaugua kwa ajili ya siku hiyo.

¹⁶¹ Sasa, tunaona hapa ya kwamba Mtu huyu, mara walipozungumza na Ibrahimu, ninawatakeni mwone, wawili wao walishuka kwenda Sodoma waone kama wangeweza kupata angalau watu kumi wenye haki katika . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . taifa la watu. [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . nao wasingeweza kufanya hivyo, lakini Mmoja alibaki nyuma. Sasa, usikose hili: Mmoja alibaki nyuma na kuzungumza na Ibrahimu.

¹⁶² Yule aliyebacki nyuma alimpa Ibrahimu ishara. Naye Yesu alirejea kwenye ishara hiyo na kusema ingekuwa vivyo hivyo katika siku za Mataifa. Sasa, tumekuwa tukichukua kote katika hili juma, kile Yesu alichokuwa, akiwaonyesha watu ishara Yake ya Kimasihi, lakini hakufanya hivyo hata wakati mmoja mbele ya Matai-... [Sehemu tupu kwenye kanda.]...?... kama tu walivyokuwa na miaka elfu nne. Lakini sasa, sisi ndio tunamtazamia Masihi ajaye. Sasa, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile.

¹⁶³ Sasa, angalia kile Huyu alichofanya, Yule aliyebacki nyuma pamoja na Ibrahimu, alimpa ishara, basi angalia hiyo ishara ilikuwa ni nini. Sasa, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," sasa watu wa kiroho, iweni na kicho kabisa hapa, nanyi, nanyi mlio kwenye ghorofa ya chini, roshani ya kwanza, na roshani ya pili, kumbukeni, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Ni wangapi wanaosema, "Amina," kwa hilo? Hivyo ndivyo... [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

¹⁶⁴ Sasa, hebu tuone kilichotukia. Kwa maana siku... Sasa, kumbukeni, siku za Sodoma zilikuwa kabla tu ya ulimwengu kuangamizwa, ama, ule—ule uovu uliangamizwa kwa Moto. Sasa, mnaamini ulimwengu utaangamizwa kwa moto katika kuja Kwake? Biblia ilisema hivyo, mbingu zote na nchi zitawaka moto. Watu watajiangamiza wenyewe, maana Mungu haharibu chochote, mwanadamu hujiangamiza mwenyewe kwa maarifa yake, werevu wake, elimu yake, daima amefanya hivyo.

¹⁶⁵ Aliumba baruti, akaumba mabomu ya atomiki, magari, hayo ndiyo yaliyomwua. Mnaona? Sasa, angalieni, yeye atauangamiza ulimwengu mzima kwa maarifa yake mwenyewe, mti ule katika bustani ambapo aliuacha Mti wa Uzima apate kula kutoka kwenye mti huo wa maarifa, sayansi, amekuwa akiupanda tangu wakati huo.

¹⁶⁶ Angalieni sasa, tunaona ya kwamba—ya kwamba Ibrahimu, wakati alipofikia mahali hapa katika—katika maisha yake ambapo ilimbidi kuona ishara hii kuu ikitukia... Yesu alirejea, kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.

¹⁶⁷ Sasa, angalieni, daima kuna matabaka matatu ya watu, ambayo ni waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini, daima; dhambi, na *wanaokiri* kuwa Wakristo, na Wakristo halisi. Nao sikuzote wametengana.

¹⁶⁸ Sasa angalieni, Sodoma ilikuwa ni wenye dhambi, walikuwa wamepotoka, kama tu ulimwengu ulivyo siku hizi. Sehemu kubwa ya taifa hili imekwisha kabisa. Na kama nilivyosema, tunajazwa tu na masega ya ukomunisti, na kila kitu, kila *itikadi*.

¹⁶⁹ Kama, wengi wenu, kama mngeweka Rais mwenye haki katika kila jimbo katika Marekani yote, ingali imekwisha, kamwe halitasimama tena, BWANA ASEMA HIVI. Mwaka wa 1956 lilipiga hatua yake ya kufisha, sasa, nalo likashika njia yake vizuri yapata miezi mitatu iliyopita. Sasa, limekwisha, liandike katika Biblia yako uone kama ni kweli.

¹⁷⁰ Mwaka wa 1933, asubuhi moja, huku nikienda kwenye maskani ya Kibaptisti, nilishikwa na usingizi mwepesi, nikaona ono, Niliona Rais Roosevelt atachangia kuuongoza ulimwengu kwenye vita vya ulimwengu, nikalisimulia asubuhi hiyo; walitaka kunifunga kwa ajili yake.

¹⁷¹ Nami nikasema, “Wataingia vitani na Ujerumani.” Miaka kumi na mmoja kabla ya Ngome ya Maginot kujengwa, nilisema, hapo katika ono lilo hilo, “Niliona Ujerumani imezingirwa kwa zege.” Nayo Marekani ilipata pigo la kutisha sana kule, na wengi wenu ninyi wavulana mnajua kilichotukia, mliokuwa kule.

¹⁷² Angalieni, nilisema, “Mussolini anajitokeza kama dikteta, atafanya uvamizi wake wa kwanza Ethiopia, lakini, ataiteka Ethiopia, bali mwisho wake utakuwa wa aibu, wote wawili yeye na mwanamke huyo.” Nao wakawanyonga miguu juu, huku nguo zake zikining’inia kichwani mwake mtaani, na kuwatemea mate.

Nikasema, “Sayansi itaimarika.”

¹⁷³ Nikasema, “Jambo lingine, taifa limewaruhusu wanawake kupiga kura, moja ya fedheha mbaya sana waliyofanya.” Kisha nikasema, “Katika kupiga kura watamchagua mtu asiyefaa.” Sasa, mimi si wa Democrat wala Mrepablikani, mimi ni Mkristo, pande zote mbili zimeoza. Lakini walifanya kosa lao baya sana hivi majuzi, wanawake walifanya kazi hiyo.

¹⁷⁴ Na jinsi ninyi watu weusi mngeweza kuuza haki yenu ya mzaliwa wa kwanza kwa kitu kama hicho, wakati damu ya doa la Abraham Lincoln iko kule juu kwenye vazi hilo! Mungu aturehemu! Nisaidie, Bwana. Loo, jamani! Labda sikupaswa kusema hilo, lakini tayari nimekwisha kulisema. Kumbukeni!

¹⁷⁵ Loo, inawezekanaje? Siku zangu kama mwinjilisti zititimia hivi karibuni, siwezi kuwa wa kinabii na mwinjilisti, pia, nitaondoka hudumani; hiyo ni katika Roho, sasa. Hivi karibuni Yeye ataniita, nitaondoka kwenye huduma ya uinjilisti, kisha atanitumia kama mwonaji Wake.

¹⁷⁶ Nina shida gani kwa vyovyote vile? Nilikuwa wapi? Naam, Mwanzo 18. (Mlipata Jeni hiyo?) Mwanzo 18, ninaamini nilikuwa nikizungumzia, basi, la, nilikuwa kwenye yale Yeye aliyoniambia yangetukia.

¹⁷⁷ Ndipo akasema, “Sayansi itaongezeka, mpaka itafikia mahali hata watakamilisha motokaa inayofanana na yai, kabla ya wakati wa mwisho.” Ndipo nikaiona, kisha nikasema, “Wataidhibiti kwa kifaa cha namna fulani cha usukani

ambapo haiwabidi kuugusa wao wenyewe. Niliona familia ya Kimarekani, ikishuka kwenye barabara kubwa, pana, ikicheza karata katika gari lililofunikwa kwa kioo, lililofanana na yai.” Wanalo sasa hivi, mliona kwenye televisheni hapa si muda mrefu uliopita, wanalo.

¹⁷⁸ Ndipo nikasema, “Kisha nikamwona mwanamke fulani mashuhuri, mwenye nguvu akiinuka Marekani.” Maana hili ni taifa la mwanamke, picha ya mwanamke kwenye pesa, zaidi, kila kitu hapa ni *mwanamke*. Mnaona? Hiyo ni kweli, yeye ni mungu mke. Si ninyi wanawake Wakristo, ninazungumza juu ya, hebu maskini kipusa ashuke barabarani hapa akiwa na kaptura hizi zote, na kadhalika, anaweza kuliletea madhara zaidi Kanisa la Mungu aliye hai miongoni mwa wanaume kuliko vilabu vyote vya pombe haramu vilivyoko kote nchini. Hiyo ni kweli.

¹⁷⁹ Hili ni, Marekani ni taifa la mwanamke, lina picha zake, namba yake ni kumi na tatu, koloni kumi na tatu, milia kumi na mitatu, nyota kumi na tatu, kumi na tatu hivyo, kila kitu ni kumi na tatu, kumi na tatu, kumi na tatu, na mwanamke. Mnaona?

“Ndipo nikaona mwanamke mashuhuri akiinuka, mwenye sura nzuri, lakini moyo katili, mwovu.” Na huyo atakuwa ni kanisa, nalo liko njiani sasa.

¹⁸⁰ Ndipo nikaona wakati wa mwisho ambapo Marekani ilionekana kama lundo kubwa la mawe yaliyopasuliwa na mambo kama hayo, imelipuliwa tu, ikifuka moshi, kila mahali. Matano ya hayo yametukia, mawili yako njiani. Hiyo imekuwa ni miaka ishirini na mmoja iliyopita, mnaona, wakati ilipobashiriwa. Kama matano ya hayo yametimia kikamilifu, hayo mengine mawili hayana budi kutimia; ninayaona yakija barabarani sasa.

¹⁸¹ Loo, tubuni na kuikimbia ghadhabu ijayo, enyi Kanisa la Mungu aliye hai! Rudi kwenye Injili halisi, rafiki. Ninyi Wamethodisti, ninyi Wabaptisti, ninyi Wapentekoste, ninyi wengine mgeukieni Mungu kwa moyo wenu wote, kwa maana saa zenu ni fupi.

¹⁸² Mwanzo 18, kabla tu ya Moto kushuka, Malaika huyo alisema, ama, Mtu huyo katika mwili wa kibinadamu, Mtu wa kibinadamu akila na kunywa kama mtu wa kawaida, bali hata hivyo alikuwa ni Mungu, Yeye alikuwa Yehova Mungu. Angalia Biblia uone kama sivyo, Yehova Mungu katika mwili wa mwanadamu. Iliwakilisha nini kulingana na Maneno ya Yesu Mwenyewe? Mungu angewakilishwa katika mwili wa mwanadamu wakati wa mwisho kabla ya moto kushuka, Roho Mtakatifu akirudi Kanisani, amekuwa akiingia kwa miaka arobaini au zaidi, akitawala Kanisa.

¹⁸³ Jambo la mwisho lililotukia ni lipi? Sasa, kumbukeni, siku chache tu kabla ya hapo, jina la Abram ilikuwa limebadilishwa likawa Ibrahimu, na Sarai likawa Sara. Basi mwangalie hapo

aliposema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Mgeni, mavumbi nguoni Mwake, akila nyama, akinywa maziwa.

Akasema, “Mbona, yeye yuko hemani nyuma Yako.”

¹⁸⁴ Angalieni hiyo ishara, Yeye alisema, “Ibrahimu, *Mimi...*” Loo, jamani! Mnaona Huyu alikuwa ni Nani? “*Mimi* nilikupa wewe ahadi, nitakurudia kulingana na ahadi Yangu. Nilitoa ahadi, Mimi Ndiye niliyeifanya.” Mungu ndiye aliyetoa ahadi. “Nitakuzuru.” Kwa maneno mengine, “Siku ishirini na nane tu zaidi, na mambo yatakuwa tofauti kwa Sara, nami nilikupa ahadi, kwa hiyo nitakuzuru kwa muhula wake, utampata mtoto huyu.”

¹⁸⁵ Naye Sara, akiwa hemani nyuma Yake, alisema—kasema, “Mimi, mwanamke mkongwe...” Samahani, akina dada, mimi...kuelezea jambo hili. Kama mume na mke, “Mimi, mwanamke mkongwe, bado ningekuwa na raha na...naye mu—mume wangu, huko nje, mzee, pia, mwenye umri wa miaka mia moja, nami hapa nina tisini,” maskini mama wa nyanya wa nyanya wa nyanya, shali ndogo na fimbo, “ati niwe kama msichana, naye mume wangu kama kijana mwanamume ku—kupata watoto? Mbona,” kasema, “haiwezekani.”

¹⁸⁶ Na huyo Malaika, si Malaika, Mungu katika mwili wa kibinadamu huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, Biblia inasema waziwazi alikuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema nyuma Yake, kasema, “Mbona Sara akacheka moyoni mwake, akisema, ‘Hakika mambo haya hayawezi kutimia?’”

¹⁸⁷ Yeye alijuaje alikuwa hemani? Ama alijuaje kama jina lake lilikuwa Sara? Alijuaje kwamba alicheka? Pia alijuaje mawazo yaliyokuwa niani mwake wakati aliwazia niani mwake? Ilikuwa ni Roho yule yule aliyekuwa juu ya Yesu aliyetambua mawazo yao. Mnaona?

¹⁸⁸ Naye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Hiyo ni kweli? Ishara ya mwisho waliyowahi kupata kabla ya ule Moto kushuka, ulishuka mara moja, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho waliyopata. Basi angalieni, Yeye alisemaje hivyo, na ni kwa nini aliita Sodoma dhahiri? Hili hapa, iweni makini mkalipokee: Huyu alikuwa ni Ibrahimu na huu ni Uzao wa Ibrahimu, Yeye hana budi kumpa Uzao kitu kile kile alichompa Ibrahimu, kwa kuwa ile ahadi ilikuwa kwa Ibrahimu na Uzao baada yake pia.

¹⁸⁹ Ee Mungu! Mnaona ninalomaanisha? Mnaona yale Biblia isemayo? Hiyo ndiyo sababu hawa Waorthodoksi wakuu sana, maarufu wananinii...kamwe hawaipati.

¹⁹⁰ Sasa, angalieni, mnasema, “Je, watapata ninii...?” Hakika. Kulikuwa na Lutu, Orthodoksi, na Billy Graham wa kisasa, ndipo mtu mwingine akashuka akaenda kule

kuwahubiria, kamwe hakufanya miujiza yoyote, kuwapofusha tu, ambapo, kuhubiri Injili humpofusha asiyeamini. Hiyo ni kweli. Waliopofushwa walikuwa wasioamini; vema, ilikuwa ni kivuli.

¹⁹¹ Sasa, wanasema ya kwamba Billy Graham, yule mwinjilisti mashuhuri siku hizi, anayewaendea nanii, mwinjilisti wa Kibaptisti, wanasema, loo, hao wenye dhambi na wasioamini wanasema, “Loo, si kitu ila lundo la upuuzi.” Sivyo! Billy Graham ni mtu wa Mungu, ndivyo hakika, na Oral Roberts, na hao jamaa, watumishi mashuhuri wa Mungu, waliochaguliwa na Mungu. Msimhukumu Billy Graham kwa sababu yeye si Mpentekoste, hawezi kuwa Mpentekoste.

¹⁹² Angalieni, wakati Mungu, hili hapa jambo fulani, natumaini halitawasonga roho, lakini angalieni, wakati Mungu, kabla hajamfanya Ibrahimu baba wa mataifa, Yeye alibadilisha jina lake kutoka Abram u likawa Ibrahimu. Hiyo ni kweli? Kaweka h-i-m-u mwishoni mwake, h-i-m-u. Kwa sababu gani? Ataleta kupitia kwake baba wa mataifa. Alichukua sehemu ya Jina Lake Mwenyewe, *Elohimu*, na kumfanya *Ibrahimu*.

¹⁹³ Sasa, mkitaka kujua kama Billy Graham . . . angalia mwisho wa jina lake, G-r-a-h-a-m. Mnaelewa? Vema. Sasa, mnaona, kila kitu hakina budi kuwa kikamilifu, na ni kikamilifu, wale wasiokiona wamepofushwa. *Ibrahimu*, hilo lilikuwa ndilo jina lililotolewa, jina hilo halikutokea mpaka kwenye wakati tu wa mwisho; vivyo limeinuka. Angalia jina hilo likiishia, h-a-m, *Ibrahimu*, *Elohimu*, mnaona, *Graham*, angalieni sasa, kwenye wakati tu wa mwisho. Loo, tungeweza kulifafanua zaidi kidogo ya hapo, lakini huo ni umbali wa kutosha kwenu kujua.

¹⁹⁴ Angalieni sasa, tunapoangalia wakati wa mwisho unaokuja, sasa, Yeye aliahidi ya kwamba hilo lingekuwa ni nini? Kabla tu moto haujashuka. Sasa, loo, kwenu ninyi watu, hii hapa ahadi kuu. Angalieni, wakati alipompa ishara hiyo, Yeye alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijiandaa, sasa. Mara baada ya hilo Yeye alifanya nini? Alimwandaa Ibrahimu na Sara kumpokea mwana ajaye aliyeahidiwa. Alifanya nini? Alimbadilisha Sara na Ibrahimu kutoka mzee na mwanamke mkongwe, akawarudisha kuwa kijana mwanamume na kijana mwanamke.

¹⁹⁵ Unasema, “Ndugu Branham, sivyo ilivyo.” Vema, tutaona tu kama ndivyo ilivyo ama sivyo. Huwezi kusoma Biblia kama gazeti, ni Waraka wa upendo.

¹⁹⁶ Maskini mke wangu huko nyuma, wakati sisi, ninapoenda ng’ambo, sasa vipi kama nilimwendea . . . ? Hapo ndipo inakubidi kuachana na mengi ya haya, “Siwezi kufanya *hiki*, kwa sababu ninakiri *hiki*. Siwezi kufanya *hiki*.” Kama unataka kukifanya, afadhali ukifanye, bila shaka. Hebu wewe, uliondoe moyoni mwako, ni upendo, neema inayofanya hilo.

¹⁹⁷ Vipi kama ni—nilianza kwenda ng'ambo, naye Bibi Branham *pale* akasema, akanijia, na kusema, "Sikiliza hapa!"

¹⁹⁸ Niseme, "Sikiliza, Bibi Branham, usiwe na waume wengine, mimi ndiye mumeo. Usiwe... Kama nikisikia umekuwa na waume wengine zaidi, nitakutaliki nitakaporudi."

¹⁹⁹ Angesema, "Ngoja kidogo, mwanaume wangu mpendwa! Usiwe na wengine, wake zaidi, pia, kwa sababu kama—kama—kama ukiwa na wake wengine zaidi, nitakutaliki utakaporudi." Sasa, hiyo si inekuwa ni nyumba?

²⁰⁰ Hivyo ndivyo kanisa linavyojaribu kuwa kwa Mungu, "Mimi ni Mpresbiteri." "Mimi ni Mpentekoste." Loo! Mnaona? Hakuna kitu, "hakuna kitu," kilicho sahihi.

²⁰¹ Angalieni, tunafanya nini? Ninampenda, yeye ananipenda. Tunapiga tu magoti na kuomba, nami ninamwomba Mungu amsaidie, naye anamwomba Mungu anisaidie, ninamwaga kwa busu, na kwenda ng'ambo, hilo latosha. Haimbidi kuwa na hofu juu yangu, ninampenda kupita kiasi; sina hofu juu yake, yeye ananipenda kupita kiasi. Maadamu tunapendana namna hiyo tutakuwa sawa.

²⁰² Nawe huna budi kumpenda Mungu. Ataniandikia barua, naye atasema, "Mpenzi Billy, ndiyo kwanza niwalaze watoto kitandani. Naye Sara, leo, alifanya *hivi-na-hivi*. Naye Rebeka, na wote namna *hii*, na ninii tu..." Mnaona? Anasema hayo kwenye karatasi, lakini ninampenda sana naweza kusoma katikati ya mistari, ninajua kile anachozungumzia. Mnaona? Ninampenda.

²⁰³ Hivyo ndivyo inavyokupasa kuwa na Mungu, huna budi kumpenda Mungu, ndipo unaweza kusoma katikati ya mistari na kuona kile anachomaanisha. Ameyaficha machoni pa wanafunzi werevu wa seminari, na kuwafunulia watoto wachanga watakoajifunza, hivyo ndivyo alivyosema; Yesu alimshukuru Mungu kwa kufanya hilo. Sasa, haihitaji elimu, inahitaji maisha yaliyosalimishwa.

Sasa, hatuna budi kuharakisha, nimepita sana, lakini sina budi tu kuelezea jambo hili Bwana akipenda.

²⁰⁴ Angalieni sasa, upendo, angalieni, sasa hebu tulichukue tu. Mnasema, "Sasa, Ndugu Branham, hebu kidogo, Yeye hakufanya hivyo."

²⁰⁵ Vema. Mara baada ya Ibrahimu kupewa ishara hii, yeye mwenyewe, nayo itapewa Uzao wake, nasi tunaona hayo yote yakitendeka, sasa ni kitu gani kinachofuata kwa ajili ya Kanisa basi? Kama Yeye, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho aliyompa Ibrahimu kabla ya Moto kushuka na kuangamiza uovu, basi itakuwaje kwa Uzao Wake? Jambo lile lile. Alifanya jambo lile lile. Yeye alifanya nini? Alimwita, akampa agano.

²⁰⁶ Ni nani anayekuita? Baadhi ya watu walisema, "Nilimtafuta tu Mungu na kumtafuta Mungu." Kamwe hukumtafuta, hakuna

mtu mwingine aliyewahi kumtafuta; ni Mungu akimtafuta mwanadamu, si mwanadamu akimtafuta Mungu. Hakuna mtu amtafutaye Mungu, Mungu humtafuta mwanadamu. Hilo lilithibitika katika bustani ya Edeni, badala ya kukiri, alikuwa akijificha, Mungu alikuwa akimtafuta.

207 Na jambo lingine, mliona? Mungu kamwe hakumtuma Malaika kumtafuta mtoto Wake aliyepotea, Yeye alikuja Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu Yesu alifanyika, Mungu, mwili miongoni mwetu. Mungu alikuja Mwenyewe kumkomboa mtoto Wake. Ilikuwa ni kazi ya mwanamume, hakuna mtu angaliweza kuifanya ila Yeye, kwa hiyo alikuja kumkomboa mtoto Wake Mwenyewe. Na hiyo ndiyo sababu Yehova alifanyika mwili katika Mwanawe apate kufa kwa dhambi iliyowekwa juu Yake kumkomboa mwenye dhambi.

208 Sasa, kwa makini, hebu tumfuate kwa dakika moja. Huyu hapa Ibrahimu. . . Huenda usikubaliane na hili, hilo ni sawa, bali ninataka tu kuwaambia mawazo yangu mwenyewe. Mnaona? Jambo la pili tu lililopaswa kutukia, kumpokea mwana huyu aliyeahidiwa ilimbidi kumfanyia Ibrahimu jambo fulani. Sasa, tunajua ya kwamba ilimbidi kumrutubisha Sara. Hiyo ni kweli?

209 Vema, katika—katika siku hizo wanawake hawakuvuta sigara, kwa hiyo ili—iliwabidi kumlea mtoto wao kwa titi, wasingeweza kuwalea kwa maziwa ya ng’ombe, hawakuwa na chupa za afya na za usafi siku hizo, kwa hiyo wao, ilibidi mama amlee mtoto wake mchanga. Vema sasa, ili kufanya hivyo, mishiya ya maziwa kwenye titi la huyo mwanamke ilikauka kwenye umri wa miaka mia moja.

210 Halafu jambo lingine, samahani, kusanyiko lililochanganyikana, mnamsikiliza daktari, mimi ni ndugu yenu, sikilizeni, jambo lingine, mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja angewezaje kupata utungu wa kuzaa? Ungemwua. Ingembidi kumfanya upya. Vema, Mungu haninii. . . Halafu mwangalieni Ibrahimu, sawa na aliyekufa, mtu mwenye umri wa miaka mia moja akirutubika? La, Yeye aliwabadilisha wakawa kijana mwanamume na mwanamke.

211 Mnasema, “Je, unaweza kuthibitisha hilo?” Naam, bwana. Walisafiri kutoka huko wakaenda moja kwa moja kwenye nchi ya Wafilisti hadi Gerari, maili mia tatu. Hiyo ni safari ndefu kweli kwa nyanya na babu mwenye mabega yaliyoinama, na masharubu yakining’inia chini namna *hii*, umri wa miaka mia moja.

“Loo,” mnasema, “waliishi muda mrefu zaidi.”

212 Ngoja kidogo hapa, ninaangalia moja kwa moja kwenye Maandiko, “Na wote wawili walikuwa na umri mkubwa sana.” Hiyo ni kweli.

213 Na walipofika kule chini, mnajua nini? Abimeleki, mfalme wa Gerari, alikuwa akitafuta mpenzi. Na hao wanawake wote

warembo wa Kifilisti kule, lakini alipomwona nyanya wa nyanya wa nyanya akiwa na shela yake ndogo na maskini kofia yake, alimpenda, “Huyo ndiye ambaye nimekuwa nikimngojea.” Mnaona jinsi linavyoonekana la kucheakesha? Ni la kucheakesha. Yeye...

Ndipo Ibrahimu akasema, “Nakuomba useme wewe ni dada yangu, kwa sababu una sura nzuri.”

214 Yeye alifanya nini? Aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Yeye atafanya nini kwa...? Kwa nini ilimbidi kufanya hivyo? Kusudi waweze kumpokea mwana aliyeahidiwa. Na hilo ndilo jambo linalofuata katika utaratibu kwa ajili ya Kanisa. “Sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana hatutawatangulia wale waliokwisha kulala mauti,” kwa kuwa tutabadilishwa katika dakika moja kumpokea Mwana aliyeahidiwa.

215 Yeye atakuja wapi, hapa chini duniani? La, juu hewani. Hatukutani na Yeye humu duniani, wala tusingeweza kukutana Naye katika miili ya namna hii, hatuna budi kubadilishwa, na kumlaki hewani. Loo, kweli ninajisikia kubarikiwa! Mnaona? Mwili huu utabadilishwa katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho, nasi tutanyakuliwa pamoja kumlaki Bwana, jambo linalofuata kwa Uzao wa Ibrahimu. Wanapata ishara yao ya mwisho, upambanuzi kama tu ulivyokuwa, siku za Yesu, hiyo ndiyo ishara ya mwisho kwa Kanisa.

216 Kumbukeni, liandikeni, huenda nikawa nimeondoka, angalieni kama ni kweli ama si kweli, ishara ya mwisho ya Biblia. Sasa, tunaona ya kwamba hiyo ilikuwa tu kabla ya jambo hilo kutukia. Halafu nini? Tunaona, mara baada ya jambo hilo, hatuna wakati wa kuendelea mbele zaidi, mtoto Isaka akazaliwa.

217 Sasa, ninafunga. Vipi kuhusu, wakati alipokuwa na umri wa kama miaka kumi na miwili, Mungu alimwambia Ibrahimu, zaidi sana hivi: “Kutakuwa na mkutano wakati fulani huko Richmond, Virginia, Marekani, ninataka kuwafanya watu wajue ya kwamba nina hakika kabisa yale ninayofanya. Nataka umchukue mwana huyo, mwanao wa pekee uliye naye, umpeleke huko juu mlimani ukamwue.”

218 Ibrahimu akasema, “Naam, Bwana.” Kwa maana alimpokea kama mtu aliyetoka kwa wafu, alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba aliweza kumfufua, kumfufua, hasa, kutoka kwa wafu.

219 Kwa hiyo Yeye alifanya nini kulifanya lithibitishwe kwa Kanisa Lake kupitia nyakati zote kwamba Yeye hutimiza ahadi Yake? Nao Uzao wa Ibrahimu, haidhuru wako katika hali gani, wangali wanaamini ya kwamba Mungu hutimiza ahadi Yake. Basi Yeye alifanya nini?

220 Alimchukua maskini Isaka, wakaenda safari ya siku tatu. Sasa, karibu mtu yeyote, kijana kama Ibrahimu alivyokuwa wakati huo, aligeuka akawa mtu mwenye umri wa kama miaka ishirini na mitano, umri wa miaka thelathini, yeye na Sara, angeweza kutembea... Ninaweza kutembea maili thelathini, nilikuwa nikishika doria huku nikiwa mlinzi wa wanyama pori, ningetembea maili thelathini siku yoyote, nasi tuna miguu ya petroli siku hizi, mbali na kile walichokuwa nacho. Usafiri wote waliokuwa nao ulikuwa wa ama kupanda maskini nyumbu au kutembea.

221 Nao wakaenda safari ya siku tatu, ndipo basi akainua macho yake, na kuona ule mlima, ambapo ono lilimwonyesha, kwa mbali, ndipo akafika mlimani. Alipofika kule, aliwaambia watumishi, "Ninyi kaeni hapa," sikilizeni hili, Mwanzo 22, "ninyi ngojeni hapa wakati mimi na mvulana huyu tukienda kule kuabudu, nasi tutarudi." Loo, hilo linanifanyia tu jambo fulani!

"Ibrahimu, unajua yale uliyosema? Unapanda kwenda kule kumwua. Utarudije, wewe na yeye?"

"Mimi na huyu mvulana tutarudi."

222 Sasa angalieni, Yeye aliweka kuni begani mwa Isaka, mfano wa Uzao wa kweli, Yesu, apate kutufanya Uzao wa Ibrahimu, alichukua kuni za dhabihu za kulalia, juu ya mabega Yake Mwenyewe, wakati alipopanda Golgotha.

223 Wakapanda juu ya mlima, na hapo wakatandaza hizo kuni, na kuwasha moto, na kadhalika, mtoto Isaka akaona shaka, akasema, "Baba?"

Kasema, "Mimi hapa, mwanangu."

Akasema, "Hizi hapa kuni, na huu hapa moto, na hii hapa madhabahu, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa ajili ya sadaka?"

224 Mnafikiri baba huyo mzee aliwaza nini? Akasema, "Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo." Amina. Hiyo ndiyo sababu alimwita *Yehova-Yire*. "Bwana atajipatia Mwenyewe mwana-kondoo kwa ajili ya dhabihu."

225 Naye maskini Isaka, yeye akasema, "Geuka, Isaka," Isaka alijua wakati huo. Basi angalieni, akijisalimisha kwa mauti, kama tu Yesu alivyofanya, ule Uzao wa kweli. Akamvuta, na kuifunga mikono yake, miguu yake, akamlaza juu ya madhabahu, akasukuma nyuma maskini nywele zake nyeusi, na macho yake madogo, ya hudhuri yakiimetameta.

226 Mama atasema nini? Hawezi kuwazia jambo hilo, huna budi kufanya yale Mungu aliyosema.

227 Mama anasema, "Usishuke uende miongoni mwa hao watakatifu wanaojibingirisha." Usiamini hilo, fanya yale Mungu asemayo.

228 Daktari anasema, “Huwezi kupona.” Usiamini hilo, amini yale Mungu asemayo. Unaona?

229 Akasukuma nyuma nywele zake, akatwaa kisu, akakichomoa kutoka kwenye ala yake, akakiinua, naye akawa tu tayari kumdunga kisu mvulana wake mdogo amwue. Ndipo alipoinua mkono wake katika utii mkamilifu, Roho Mtakatifu akamshika mkono wake, kasema, “Ibrahimu, ondoa mkono wako, ninajua ya kwamba unanipenda, kwa maana hata hungemwachilia mwanao mwenyewe.”

230 Na yapata wakati huo, nyuma yake, ambako aliyaokota yale mawe, kondoo dume akalia, amenaswa kwa pembe zake nyikani, kichakani. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani: Huyu kondoo dume alitoka wapi? Sasa, yeye yuko angalau maili sabini na tano kutoka kwenye ustaarabu, na wanyama wa kila namna. Naye kondoo ni chakula cha yeyote yule, simba, mbweha, na yeyote yule jangwani. Na alikuwa wapi huyo...? Huyu kondoo dume alitoka wapi? Na jambo lingine, yeye yuko huko juu kabisa mlimani ambako hakuna maji.

231 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu alimnena akawa, alikuwa na haja naye. Mnaona, haikuwa ni ono, sasa, alimchukua huyo kondoo dume, akamleta huko, na kukata koo lake, ono halitoki damu, damu ikatoka. Alichukua mahali pa Isaka, ilikuwa ni Yesu katika mfano. Mnaona ninalomaanisha?

232 Ndipo Ibrahimu akasema, “Mahali hapa pataitwa *Yehova-yire*, ‘Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu.’” Nalo likasema, “Hata katika mlima wa Bwana, hata wa leo.” Yehova-Yire tayari amejitolea Mwenyewe dhabihu.

233 Basi ndugu, dada, unasema, “Ndugu Branham, nilikuwa kwa daktari, akaniambia siwezi kuishi.” Vema, hapana shaka, ila kwamba mtu huyo wa thamani anakwambia kila kitu anachojua kwamba ni kweli, bila shaka, bali anajua tu kama mwanadamu. Waliniambia miaka thelathini na miwili iliyopita, nilikuwa na chini ya dakika tatu za kuishi, moyo wangu ulikuwa ukipiga tu mara kumi na saba kwa dakika. Vema. Lakini Yehova-Yire, Yeye alitoa Dhabihu nami nikaikubali.

234 Yehova-Yire yuyo huyo ana Dhabihu iliyotolewa kwa ajili yako, leo. Je, utaikubali? “Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Loo, ewe Uzao wa Ibrahimu, hivi hutaipokea Dhabihu ya Yehova iliyoraruliwa pale Kalvari? Sehemu Yake imewekwa pale kwenye Enzi ya Mungu, kwenye mkono wa kuume, Kuhani Mkuu akikuombea unapokiri. Roho Mtakatifu yuko hapa kuendeleza Kazi Yake miongoni mwa Kanisa Lake. Amini na umpokee, sivyo?

235 Na tuinamishe vichwa vyetu. Wakati tukiwa katika maombi, kwa dakika moja ama mbili tu zijazo, kunaweza kuwako na yeyote katika jengo hili kwenye roshani ya kwanza, roshani ya pili, au kwenye sakafu kuu, mnaoweza kumwinulia

Mungu mikono yenu, sio mimi...? Kila jicho lifumbwe tafadhalini, kila mtu kimya tu awezavyo kuwa. Hapana budi uamuzi ufanywe, kuna *Kitu fulani* kinachosimama karibu nawe, ama anakwambia, “Mtoto, hivi huna furaha kwamba ulipokea Dhabihu Yangu iliyotolewa?” Au ama anakwambia, “Unanihitaji Mimi kama Mwokozi wako, nimekupa Dhabihu, utaipokea?”

²³⁶ Kama bado hujampokea, waweza kuinua mkono wako, na kumwonyesha tu Mungu, “Ninataka kumpokea”? Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe, wewe. Naam. Roshani ya pili; Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Mungu awabariki. Hakika. Vema, hilo ni sawa.

²³⁷ “Loo, Yehova-Yire, nijalie sasa. Tayari umeitoa, nami ninaikubali bure, Yesu alikuwa Dhabihu Yako iliyotolewa kwa ajili yangu, Mwana-Kondoo kwa ajili ya macho yangu, Mwana-Kondoo kwa ajili ya mwili wangu, Mwana-Kondoo kwa ajili ya nafsi yangu.”

²³⁸ Na, loo, kwenu ninyi mlio wagonjwa na wanaoteseka, moyoni mwako useme, “Yehova, nipe imani, sasa hivi, kupokea Dhabihu ambayo imetolewa kwa ajili yangu, kwa kuwa Dhabihu yangu ilijeruhiwa kwa makosa yangu, ambayo nimeipokea, na kwa kupigwa Kwake niliponywa. Sasa naja kumpokea, sasa hivi.”

²³⁹ Baba wa Mbinguni, wakati unakaribia, haitachukua muda mrefu mpaka wahudumu hapa, ndugu zangu wa thamani, watakuwa mimbarani mwao, watakuwa wakitoa jumbe kuu, usiku wa leo. Ninaomba wagonjwa na wanaoteseka wataponywa, na wenye dhambi wataokolewa, na watu wajazwe na Roho Mtakatifu. Jalia matokeo ya Uwepo Wako yabaki kila mahali, mpaka Yesu atakapokuja.

²⁴⁰ Sasa, katika njia hii ndogo, rahisi, Bwana, ni—nina njia mbaya sana ya kuelezea chochote, na kama nimeudhi mahali popote, Wewe nisamehe, Bwana, unajua ninii, Wewe unajua kusudi na nia yangu. Nami naomba ya kwamba utasaidia. Na hizi Mbegu chache, jalia ziingie ndani moyoni mwa watu. Jalia ilete uamsho mkuu hapa, Bwana.

Wabariki watu hawa walioinua mikono yao. Kama ule wimbo mzuri:

Wewe ndiwe Mfinyanzi;
Mimi ni udongo.
Sasa, nifinyange na unifanye, Bwana,
Sawasawa na njia Yako,
Wakati nimejitolea,
Nikingojea, mtulivu.

²⁴¹ Tujalie, Baba, wale walioinua mikono yao, wanaotaka kukumbukwa katika maombi, wanaitaka hiyo Dhabihu, imani ya kusimama na kuipokea. Jalia wafanye hivyo sasa hivi,

Baba. Jalia waokoke. Huenda nisiwaone kamwe humu duniani, liwazie, Baba. Tutatengana sasa katika dakika chache, labda tusikutane tena mpaka siku hiyo pale langoni.

²⁴² Ee Mungu, ningetaka kusimama karibu na nguzo pale na kusema, “Mnaona, si ni ajabu sasa?” Kama tu lile ono uliloonyesha, ambalo kitabu hiki kinalo, karibu sana. Tujalie, Bwana.

²⁴³ Ninawaleta Kwako kama kumbukumbu za Injili ambayo imehubiriwa, na Roho Mtakatifu hapa, akiwavuta kwa Yesu. Wewe ulisema, “Wote alionipa Baba watakuja; na yeye ajaye sitamtupa nje kamwe.” Kwa hiyo jambo ndilo hilo, Baba. Walio wagonjwa, ninakuomba uwaponye. Tujalie, katika Jina la Yesu.

²⁴⁴ Sasa, ninyi mnaoamini na mnamtaka Yesu akufanye mtoto Wake halisi, inueni tu mikono yenu, huku vichwa vyenu vimeinamishwa, inua mkono wako.

Fanya upendavyo, Bwana!
Fanya upendavyo!
Wewe ndiwe Mfinyanzi;
Mimi ni udongo.
Nifinyange na unifanye
Sawasawa na mapenzi Yako,
Wakati nikingojea,
Nimejitolea na kutulia.

²⁴⁵ Mungu awabariki. Baraka nyingi, kuu za Mungu, zisizo na mwisho zikae juu ya kila mmoja wenu, tunapongojea kwa unyenyekevu, kwa utamu.

²⁴⁶ Sasa, kuna kadi chache za maombi zilizosambazwa humu jengoni, tunataka kuwaombea. Kabla hatujaita kadi za maombi, wakati tumeketi humu mkutanoni chini ya upako wa Roho Mtakatifu, Uwepo Wake mtamu umetuzunguka, ni wangapi huko nje walio wagonjwa, hapa, juu kwenye roshani, popote ulipo, ukisema, “Mimi ni mgonjwa, Ndugu Branham, Mungu anajua mimi ni mgonjwa, nami na—na—nataka, na—nataka Roho Wake Mtakatifu mkuu aje aniponye?” Inua tu mkono wako, useme, “Ni—ni—nina—ninataka Roho Mtakatifu mkuu aje aniponye.” Mungu awabariki.

²⁴⁷ Yule Malaika niliyenena habari zake juma hili lote... Je, kuna wageni wowote hapa? Inua mkono wako? Wachache tu sana. Vema, juma hili lote mmeona ninii... Mngemwamini sasa kama angefanya jambo lile lile?

²⁴⁸ Hakuna mtu hapa ndani ninayemjua, mke wangu ameketi huko nyuma kabisa, na rafiki yangu ameketi *hapa*, Ndugu Goad, hao ndio watu pekee ninaowajua, ninaowaona, isipokuwa hawa watu wawili walioketi papa *hapa*. Ninaamini walikuwa kwenye mahojiano ya faragha jana, watu hawa wawili. Nje... Ni wangapi wanaojua ya kwamba hatufahamiani? Asanteni. Iweni na imani, msiwe na shaka.

249 Sasa, kama Roho Mtakatifu atathibitisha hili kuja hapa, na kuacha...Mtainua juu...Biblia ilisema ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, na Dhabihu hiyo ilipasuliwa, unaamini Huyu alikuwa ni Yesu Kristo kwa ajili yako? Unaamini Yeye ameketi mkono wa kuume wa Mungu sasa, akikuombea unapokiri? Unaamini Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako?

250 Basi wewe omba, na kumsihi, na kumgusa, na kumwambia, useme, "Bwana, Ndugu Branham ndio kwanza atwambie ya kwamba Wewe uko hapa ndani yetu. Nami ni sehemu Yako, pia, Ndugu Branham ni sehemu Yako. Ndugu Branham ni mtumishi Wako, na sasa kama Wewe utanena tu kupitia kwake kama ulivyofanya Mwanao, Yesu...Yeye ni mwana Wako mwenye mamlaka, mimi ni binti Yako mwenye mamlaka, mwana Wako mwenye mamlaka, bali Wewe ulimtuma kwetu a—awe ishara kwetu wakati wa mwisho, alilinena."

251 Huko juu kwenye roshani, popote ulipo, sininii...popote ulipo, haijalishi, amini tu. Kama Yeye atafanya hivyo, je, utakuwa na imani nyingi na kuamini? Inueni mikono yenu, kusudi niweze tu kuona jinsi mtakavyoamini hilo. Vema. Mungu awabariki.

252 Sasa, huu ndio wakati, ndugu. Sasa, kama mtu yeyote akileta maswali, waambieni waje. Sasa, huu ndio wakati ambapo haikubidi kuwa na wasiwasi, Mungu anaposema jambo lolote, Yeye hutimiza Neno Lake. Hiyo ni kweli.

253 Sasa, kuwa na imani, usiwe na shaka, bali amini kwa moyo wako wote. Sema tu, "Bwana, jalia nikuguse Wewe," mahali popote humu ndani. Basi kama akifanya hivyo, angefanyaje? Kama tu alivyofanya wakati yule mwanamke alipogusa vazi Lake, akageuka, kasema, "Ulikuwa na kutokwa na damu, lakini imani yako imekuokoa." Mnaona? Jambo lile lile.

254 Sasa, utaamini? Hili si ni jambo kuu? Ni changamoto jinsi gani! Loo, jamani! Sema, "Je, litatukia?" Bila shaka, Yeye hashindwi.

255 Iko wapi miungu ya Baalimu? Yuko wapi mkosoaji wenu, asemaye Roho Mtakatifu si sahihi? Njoo hapa, fanya jambo lile lile.

256 Unasema, "Vema, Yesu alisema, 'Aliye mkuu kuliko huyu...'" Njoo ufanye kazi alizofanya kwanza, kisha tutazungumza juu ya kubwa zaidi, nami nitakwambia ni nini. Yesu asingeweza kuhubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulikuwa haujaja bado, hizo ndizo kazi kuu zaidi tunazofanya. Lakini fanyeni kazi zile zile alizofanya, Yeye alisema mtafanya.

Unawazia nini kuhusu tatizo hilo la shingo, mama? Unafikiri Bwana ataiponya na kuipa afya? Amefanya hivyo.

Sijawahi kumwona maishani mwangu, yeye ni mgeni kabisa kwangu mimi.

Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako. Lakini ulikuwa umeketi pale ukiomba, sivyo? Hiyo ni kweli. “Bwana, hebu iwe ni mimi.”

Ninawezaje kumwambia kile anachoombea? Huo hapo mkono wake umeinuliwa, mkono wake wa kuume kwa Mungu kwamba ni kweli. Ni kitu gani? Ati mimi? La, ni Yeye.

²⁵⁷ Huyu aliyeketi pale pamoja na Ibrahimu hakuwa ni mwanadamu, akila nyama na kadhalika namna hiyo, ilikuwa ni Mungu ndani ya Mtu huyo. Haikuwa ni Yesu, Yeye alisema, “Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu.”

²⁵⁸ Kuna mama mnene, aliyeketi moja kwa moja nyuma yake, akiniangalia moja kwa moja, amekuwa akiombea pale, tangu nilipoanza, akasema hivyo, akiombea ugonjwa huo wa moyo. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa, unaamini? Vema, ugonjwa wako wa moyo umekwisha. Amini, usiwe na shaka.

²⁵⁹ Aisee, “Mbona unaonekana hivyo?” Nilikuwa nikiiangalia ile Nuru, iko juu ya mama huyu papa hapa. Yeye hajiombei mwenyewe, bali anamwomba dada yake, ana ugonjwa wa moyo. Yuko hospitalini, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ulikuwa unamwomba. Kama hiyo ni kweli pungu mkono wako *hivi* kusudi watu waone. Ninawezaje kukwambia kile unachoombea? Mungu anayesikia maombi, anayejibu maombi. Unaamini anatoka, akiwa mzima sasa? Uligusa kwa ajili Yake. Hiyo ni kweli.

²⁶⁰ Unaombea macho yako, ingawa umevaa miwani, uliyeketi hapo, huyu mama papa hapa mwishoni aliyevaa koti hili jeupe. Naam. Ulikuwa umeketi hapo ukiombea macho yako, sivyo? Kusudi upate kujua: Huyu mama aliye karibu nawe anaombea mishipa iliyovimba. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mama aliyeketi karibu naye, anaombea ugonjwa wa wasiwasi ambao amekuwa nao kwa muda fulani. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona?

²⁶¹ Unaamini? Unasema, “Ndugu Branham, Yule Malaika alikuwa amegeuza mgongo Wake. Je, Yeye atatenda vivyo hivyo? Unatuangalia usoni, huenda unasoma mawazo yetu.” Vema, nitageuza mgongo wangu basi. Angalieni kama ni Malaika yule yule. Sasa, mimi si Yeye, ni Roho Wake.

²⁶² Sasa, kama mnaniangalia, angalieni imesimama hapa. Mnaiona hiyo Nuru? Sasa, kuna mwanamke, mnamwona akiketi? Ameketi, angekuwa *hivi* nyuma yangu. Anaugua ki—kivimbe kooni mwake, naye ana mvulana, naye ana ugonjwa wa mapindi. Jina lake ni Bibi Mitchell. Simama, Bibi Mitchell, amini kwa moyo wako wote.

263 Mama, sikujui, kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako huku na huku *hivi*. Je, hilo ndilo ulilokuwa ukiombea, alilokwambia? Vema. Lipokee sasa, nenda nyumbani, uwe mzima. Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini?

264 Kuna mwanamume aliyeketi moja kwa moja nyuma yake. Yeye akiangalia huku, ninauona sasa hivi. Ana ugonjwa wa mgongo, pia, alifanyiwa upasuaji kwa ajili ya ugonjwa wa mgongo. Ana uvimbe wa pua ambao ndio uliomfanya aamini, ana ugonjwa wa mapindi. Hiyo ni kweli. Bw. Bush, kwa nini usisimame na kukubali uponyaji wako, pia?

Unaamini?

265 Kama sikujui, bwana, pungu mikono yako huku na huku, kama—kama hatufahamiani. Je, hilo ndilo ulilokuwa ukiombea? Punga mikono yako huku na huko *hivi*, kama wewe... kama ilikuwa ni kile, ulikuwa ukiomba. Vema. Mungu akubariki. Nenda nyumbani, pokea uponyaji wako.

Yeye ni Mwokozi wa ajabu, sivyo?

266 Kuna mtu aliyeketi pale kwenye roshani, anaugua ugonjwa wa mkamba. Bw. Brown, simama. Haya basi. Sikujui, sivyo, bwana? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Umeponywa, Yesu Kristo anakuponya.

267 Papo hapo ameketi mama mmoja akimwombea ndugu yake aliye na kansa. Amini, ataponywa kama ukiamini hilo. Unaliamini kwa moyo wako wote? Vema, unaweza kuupokea.

Ugonjwa wa moyo, wasiwasi, moja kwa moja mwishoni, yabisi kavu uliyeketi moja kwa moja nyuma yake. Unaamini kwa moyo wako wote?

268 Sasa, Yeye yuko hapa? Mnaamini Yeye yuko hapa? Imeenea kote jengoni, ikiwaonyesha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, kwenu nyote, inaonekana kana kwamba sasa ingeweza...

269 Ni wangapi wanaojua ya kwamba maono karibu yakuue? Yesu alisema, “Naona kwamba nguvu zimenitoka.” Huyu ni Yeye. Sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, lakini inaonyesha ya kwamba Malaika yule yule, ahadi ile ile! Jambo linalofuata ni maangamizi katika taifa hili, si taifa hili tu, bali kila taifa, wakati wa mwisho umewadia, kubadilishwa kunawangojea watu.

270 Ni wangapi walio na kadi za maombi? Inua mkono wako. Ninawatakeni mninii, safu hii hapa msimame, mje moja kwa moja hapa chini. Anzeni tu kusimama, safu kwa safu, mkishuka moja kwa moja hapa.

271 Sasa, nitawaambia jambo fulani, ninataka kuwathibitishia jambo fulani. Mimi siye tu ninayepaswa kuwaombea wagonjwa,

ndugu zangu hapa wana haki kama nilivyo nayo ya kuwaombea wagonjwa, nami ninataka kuwathibitishieni.

Ndugu, njoni.

²⁷² Hamwezi kuja huku, mabwana, inawabidi kutoka nje, na kupitia upande ule mwingine, upande ule. Pamoja na kadi za maombi, mkiwa tu na kadi za maombi. Tokeni nje, kisha mje huku hivyo. Mkiwa tu na kadi za maombi sasa.

²⁷³ Ninawataka ndugu zangu wasimame hapa. Njoni hapa, ndugu, ninawatakeni, fanyeni mstari pande zangu zote mbili hapa. Njoni hapa. Ili watu hawa wapate kujua, si lazima mumngojee mtu kama Oral Roberts, ama Tommy Hicks, ama mtu fulani akipitia huku, watu hawa wamechaguliwa na Mungu kuwaombea wagonjwa. Wana haki ya kuwaombea wagonjwa kadiri nilivyo nayo, ama mtu mwingine yeyote. Mnaweza kuliona sasa hivi, katika dakika chache kama hawa kweli ni Uzao wa Ibrahimu.

²⁷⁴ Kuna mtu yeyote humu ndani aliye na kadi za maombi sasa? Kama mnazo, jitokezeni moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa, humu ndani, kisha mzunguke na kufanya mstari huo, zungukeni moja kwa moja kupitia upande wa nyuma, zungukeni moja kwa moja, na mpange mstari.

²⁷⁵ Sasa, kama hukiri imani yako katika Kristo, usije, maana itakuwa mbaya zaidi kwako, “Nenda zako, wewe, na usitende dhambi tena.” Dhambi ni nini? [Ndugu mmoja anasema, “Kuvunja sheria.”—Mh.] Kutokuamini. Kuvunja sheria ni sawa. Kutokuamini. “Yeye asiyeamini amehukumiwa” (Ati nini?) “amekwisha kuhukumiwa.” Hiyo ni kweli?

²⁷⁶ Hii, wahudumu? Vema. Naam. Uko wapi, Ndugu Hall? Huyu Ndugu Hall hapa ana huduma, yeye huwaombea wagonjwa pia, ana ibada za nchi nzima, Ndugu Hall. Nawatakeni mje humu ndani, Ndugu Hall, ninawatakeni mfanye, nyote mfanye mistari miwili, hapa.

²⁷⁷ Wote katika sehemu hii sasa mlio na kadi za maombi, njoni moja kwa moja kwenye marefu ya kanisa, mwende juu moja kwa moja, kisha mzunguke huko nyuma. Nanyi mlio kwenye roshani mlio na kadi za maombi, kama kuna yeyote wenu huko juu, shuka moja kwa moja, na uchukue mahali pako kwenye marefu ya kanisa, papa hapa nyuma ya mahali hapa, ninyi mlio na kadi za maombi, njoni mstarini.

Sasa, kama huamini, nawe si Uzao wa Ibrahimu, wala huko tayari, sasa hivi, kusema, “Yote yamekwisha, yote yamekwisha. . .”

²⁷⁸ Sasa, Mungu yeye yule aliye hapa kufanya mambo haya. . . Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ni wangapi wanaoamini ya kwamba *ni* Roho Mtakatifu? Inua mkono wako. Sasa, unajua, ungeweza kuchukua msimamo

mwingine, na kusema ilikuwa ni kitu kingine, basi hilo litakuwa kati yako na Mungu, unaona, kamwe hutasamehewa hilo. Hiyo ni kweli, Yesu alisema hivyo. Lakini kama utaamini kwa moyo wako wote!

²⁷⁹ Sasa, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, sasa, hatuwezi kuja kupitia upambanuzi, tunajua hilo. Labda, hawa ndugu hapa hawana. Mnaona? Lakini si lazima wawe nayo, unajua yale umefanya, na kilicho shida yako, kama ulitenda dhambi, mwombe Mungu akusamehe; kama huamini, mwombe Mungu akurehemu na kukufanya uamini.

²⁸⁰ Lakini ni wangapi sasa, wa ninyi watu mlio kwenye mstari wa maombi, mliosimama hapo, ninyi mlio na kadi za maombi, mliosimama mstarini, utamwinulia Mungu mkono wako, kwamba umemkubali Yeye kama Mponyaji wako? Inua mkono wako. Ninyi wengine, kama kuna wengine hapa nje ambao hawako kwenye mstari wa maombi wanaotaka kumkubali Yeye kama Mponyaji wenu, inua mkono wako. Mungu awabariki.

²⁸¹ Sasa, Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono juu ya wagonjwa watapata afya.” Hivyo ndivyo alivyosema? Vema, basi kuna namna fulani ya Ro—Roho hapa, kuna nguvu fulani zinazojua wewe ni nani, zinazojua yote kukuhusu. Hiyo si ni kweli? Anajua kila kitu. Mbona, Yeye, kama Yeye aliahidi kufanya hivyo, Yeye hutimiza ahadi hiyo, Yeye atatimiza kila ahadi.

²⁸² Sasa, kama huamini, kumbuka, usije kwenye mstari wa maombi.

²⁸³ Sasa, ndugu, nataka yapata nusu yenu mlio upande mmoja *hapa*, mshuke *hivi*. Hiyo ni kweli. Vivyo hivyo *hapa*, hiyo ni kweli, kila mmoja, mfanye mistari miwili. Hilo ni sawa. Ninyi wahudumu wawili? Loo, unawasaidia watoke jukwaani, mtu fulani hapo chini wa kuwasaidia watoke.

Sasa, kabla hujaanzisha mstari wa maombi, Billy, ngoja kidogo tu, na tuombe.

²⁸⁴ Sikilizeni, enyi marafiki, ninataka kuwaulizeni ninyi ndugu, nina imani kamili kwenu kama ndugu zangu, najua ninyi ni watu wa Mungu, walioitwa na Mungu. Ninajaribu kulijulisha kusanyiko hili ya kwamba si lazima limngojee mtu fulani aje, karama fulani maalum. Karama haziponyi, karama zinamtangaza tu Mungu. Ninyi nyote ni wahudumu mnaolijua Neno vizuri zaidi kuniliko mimi, kwa hiyo karama yako inapaswa kufanya hivyo, na hiyo ndiyo njia ya asili, amini Neno Lake. Yeye alilituma Neno Lake na kuwaponya, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Lakini basi, Mungu ni mwema sana, na hutoa ahadi kama hizo, kama—kama—kama hawawezi kuliadini Neno, basi Yeye anawaonyesha ishara kwamba ni

Yeye pale, hilo ndilo kusudi lake, hiyo ndiyo sababu nina ninyi hapa.

²⁸⁵ Na sasa, wazieni tu: Vipi kama mama yangu alikuwa amesimama kwenye mstari huo, ama vipi kama mama yako alikuwa amesimama kwenye mstari huo? Vipi kama mke wangu alikuwa kwenye mstari huo, ama wake zenu walikuwa kwenye mstari huo? Vipi kama mtoto wangu alikuwa amesimama kwenye mstari huo, na mtoto wako alikuwa amesimama kwenye mstari huo?

²⁸⁶ Enyi wasikilizaji, vipi kama mngekuwa mama yangu, au baba yangu, ndugu yangu, dada yangu, mke wangu, au mtoto? Na vipi kama huyo alikuwa, huyu *mwingine* alikuwa ni wako? Sasa, nguvu za Kanisa ni kukusanyika pamoja na kuomba. Sasa, tunaweza kuomba, na kisha tuweke mikono juu ya wagonjwa. Mnakumbuka, Petro alienda kule na kumwomba Dorka pembeni, kisha akasimama kutoka kwenye maombi yake, akaenda akamwekea mikono, naye akafufuka baada ya kufa? Tumeomba, kisha tupitie desturi ya kuweka mikono juu ya wagonjwa, kama tu kufanya ubatizo, ama chochote mnachofanya ninyi ndugu, jambo lile lile. Je, nyote mnaamini hilo kwa uchaji? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Sasa, hebu na tuinamishe vichwa vyetu. Sasa, ndugu ombeni, kila mtu.

²⁸⁷ Baba yetu wa Mbinguni, huu ndio upeo. Tumehubiri Neno Lako, ambalo ulituagiza kufanya, tumewaona wenye dhambi wakiinua mikono yao na kuwa Wakristo, tuliona wenye uvuguvugu wakiinua mikono yao na kuungana tena na Wewe katika ushirika, tuliwasikia watakatifu wakilia na kupaza sauti, tumemwona Roho Mtakatifu akitenda kazi miongoni mwetu, na kulithibitisha Neno, na kuhakikisha, kulingana na Neno nililohubiri, ya kwamba alilifanya litende yale hasa aliyoahidi litafanya.

²⁸⁸ Bwana, watu hawa wanataka kuponywa, nami ninajaribu kuwaambia, hakika tu kama unavyolifanya Neno Lako imara na kulithibitisha, tayari uweponywa, *wameponywa*. Na ukitimiza ahadi Zako juu ya jambo moja, unatimiza ahadi Zako juu ya mambo yote. Sasa, huwezi kuwaponya sasa, kwa sababu tayari wameponywa, bali tuna utaratibu mmoja zaidi wa kupitia, huo ni kuweka mikono juu ya wagonjwa, jambo lako la mwisho, Wewe, agizo la mwisho ulilolipa Kanisa, na huu ndio mkutano wa mwisho katika uamsho huu. Tunachukua agizo la mwisho, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁸⁹ Mungu, ninaomba ya kwamba kila mmoja wa hawa wahudumu hapa atatiwa mafuta sana na Roho Mtakatifu, hata kamwe hawatasahau jioni ya leo, wakati watu hawa

wanapopitia hapa. Wanaomba, Bwana, mioyo yao inawaka moto, wanataka kukufanyia Wewe jambo fulani. Kuna wengine huko nje kwenye kusanyiko, ambao hawajasimama kwenye mstari wa maombi, wanaomba. Jalia Roho Mtakatifu aliyepo na anayelijaza jengo hili sasa kwa Uwepo Wake, huko juu kwenye roshani, chini sakafuni, kila mahali, Yeye yupo hapa, jalia aje sasa, Bwana, na kututia mafuta.

²⁹⁰ Na jalia watu hawa wapakwe mafuta sana, wanaopitia hapa, mara tu, wanapofika mstarini jalia watambue ya kwamba hawaji kwa wanadamu, bali wanakuja kwa Mungu. Jalia watembe chini hapa kana kwamba walikuwa wakipitia chini ya msalaba, watoke kwenye jukwaa hili wakishangilia, kama Uzao wa Ibrahimu, wakiwa na nguvu, wakimsifu Mungu, washuke kwenye marefu ya kanisa wakimsifu Mungu, na waponywe.

²⁹¹ Jalia ndugu hawa waone makanisa yao yakikua katika nguvu na uweza kwa shuhuda zao, na wengine waingie, na mambo makuu yafanyike. Baba, tujalie. Tunawakabidhi Kwako sasa, na sisi wenyewe, ya kwamba utatutia mafuta, kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

²⁹² Sasa, kwa wote, kila mtu anayeamini, inueni mikono yenu, “Ninaamini. Ninaamini, Bwana, ninaamini.”

²⁹³ Sasa, kama upako ukiwa mwingi sana, nisipate nafasi ya *kuwaaga*, Bwana awabariki.

²⁹⁴ Kila mtu katika maombi sasa. Tayari tumeomba. Sasa, hebu na tuimbe sasa, tunapoimba, “Amini tu, amini tu,” tunapoinamisha vichwa vyetu kwa kicho, kuombeana tu sasa, tunapoweka mikono juu ya watu hawa.

Amini tu, ninii tu. . .

Njoo, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo pokea uponyaji wako.

²⁹⁵ Katika Jina la Yesu, pokea uponyaji wako, ndugu yangu. Amina. Hiyo ni kweli. . .? . . . [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . kila kitu kimeondoka. Ni mtazamo wako wa kumkaribia Mungu, hivyo ndivyo ilivyo.

Katika Jina la Yesu Kristo, pokea uponyaji wako.

Katika Jina la Yesu Kristo, upokee.

Loo, enyi Uzao wa Ibrahimu, njoni mkiamini!

Katika Jina la Yesu Kristo, pokea uponyaji wako.

Ee Mungu, mponye ndugu yangu, naomba.

Katika Jina la Bwana wetu Yesu, mponye ndugu yangu.

Katika Jina la Bwana Yesu, mponye dada yangu, Baba, ninaomba.

Mungu, katika Jina la Yesu...?...

Katika Jina la Bwana Yesu, mponye, Baba.

Katika Jina la Yesu, mponye, Baba.

Katika Jina la Yesu, ninamwombea.

Katika Jina la Bwana Yesu...?...

Katika Jina la Bwana Yesu...?...

Katika Jina la Bwana Yesu...?...

Katika Jina la Yesu...?...

Katika Jina la Yesu...?...[Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wale walio kwenye mstari wa maombi, mengi ya maneno yake hayatambuliki—Mh.]

²⁹⁶ Wote wanaomwamini sasa kama Mponyaji wao, mtamkubali sasa, kama Uzao wa Ibrahimu? Utamwamini Bwana Yesu kwa moyo wako wote? Je, sasa unataka kumkubali kwa chochote, wokovu, kwa ajili ya uponyaji, kwa ajili ya ubatizo wa Roho, ama chochote cha zaidi? Utamwamini kwa moyo wako wote? Simama kwa miguu yako basi, simama. “Kama Uzao wa Ibrahimu, kama Wakristo waaminio sasa tunamwamini Yesu Kristo.” Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Sasa, usijiombe, mwombe huyo aliye karibu nawe.

Na sisi ndugu, tutaungana pamoja.

²⁹⁷ Kama kundi moja la Kikristo, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Wapentekoste, Katoliki, chochote ulicho, tunaungana pamoja na jitihada zetu pamoja mbele za Yehova Mungu, Mwokozi wetu, Yule aliyepo sasa kujionyesha Mwenyewe yu hai baada ya miaka elfu moja mia tisa. Yuko hapa Richmond, Virginia alasiri ya leo katika umbo la Roho Mtakatifu, akijithibitisha Mwenyewe kuwa hai, Yeye sasa anawaponya, kila mmoja wenu.

²⁹⁸ Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, jalia kila nguvu za ibilisi zivunjwe, na kila mtu aponye, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. 

61-0312 Yehova-Yire
Lyric Building
Richmond, Virginia Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org